# Nipashe

Jumatano Septemba 30, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580354

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




Manara: Miquissone ataitajirisha Simba

UKURASA 24

**MTENDAJI** asimamishwa kazi madai kuwafungia wanafunzi na nguruwe

UKURASA 4



**MATATANI** tuhuma kumkata mkewe kiganja cha mkono

UKURASA 4

# Fursa sasa yanukia kwa wakulima maparachichi

JPM awaahidi kuuza mazao yao Ulaya uwanja wa Njombe ukikamilika... *Endelea uk. 2*



Aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Arusha, Amina Mollel, akiwa amelala wakati akiwaombea kura wagombea urais, ubunge na udiwani wa CCM, katika mkutano wa kampeni kwenye viwanja vya Miti Mitatu, Kata ya Tarakwa, wilayani Arumeru juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# IPP Media yang'ara tuzo za uandishi

ENDELEA UK 4



Waandishi wa habari wa kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, wakiwa wameshika tuzo na vyeti baada ya kuibuka washindi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT) zilizoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), jijini Tanga juzi. Kutoka (kushoto) ni Ashton Balaigwa, Marco Maduhu, James Kandoya, Muhidini Msamba, Sanula Athanas, Christina Mwakangale, Rahma Suleiman, Abdul Kingo na Crispin Gerald. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### ATAKA DK. MENGI AENZIWE KWA TUZO

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, amelishauri Baraza la Habari Tanzania (MCT) na wadau wa...

UKURASA WA 3

### NEC YAKUNJUA MAKUCHA WAGOMBEA KUHUSU MATUSI

ZIKIWA zimesalia siku 29 kufanyika Uchaguzi Mkuu mwaka huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewataka wagombea na vyama vya siasa...

UKURASA WA 3

### POLISI YATOA TAMKO ZITO KWA WAGOMBEA, WAFUASI

JESHI la Polisi limetoa tamko kwa wagombea na wafuasi wao likiwataka kuacha kutoa lugha za...

## Mgombea UPDP ataka viboko 100 wala rushwa

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAIKARIBISHA KMKM CHAMAZI KUONGEZA MAKALI UK 23

MAONI, KATUNI UK. 6

## HABARI KITAIFA

# Magufuli aahidi neema wakulima maparachichi

**Na Gwamaka Alipipi, NJOMBE**

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema kukamilika kwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Njombe, kutawawezesha wakulima wa parachichi, chai, mboga kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuuza kimataifa.

Amesema uwanja huo utakapokamilika ndege kutoka nchi za Ulaya zitaweza kutua na kubeba mazao hayo, wakulima kujiongezea kipato pamoja na kukuza uchumi wa taifa.

Aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na umati wa wananchi na wanachama wa CCM, waliojitokeza kumsikiliza katika Uwanja wa Polisi, akiomba kura pamoja na kueleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano.

"Wananchi wa Njombe ni wakulima wazuri wa parachichi, chai na mboga, hivyo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Njombe utakapokamilika, ndege kubwa kutoka nje zitatua na kubebea mazao yenu. Hata ndege za mizigo tutakazonunua zitaweza kufika hapa," alisema Magufuli.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali itahakikisha inakifufua kiwanda cha chai cha Lupembe ili wakulima wa zao hilo waweze kuwa na soko zuri.

AHADI NJOMBE

Aidha, Dk. Magufuli alisema miaka mitano ijayo serikali imeweka mipango thabiti ya kuhakikisha Mkoa wa Njombe unapiga hatua za kimaendeleo na kiuchumi.

Alisema Sh. bilioni 121 zimetengwa kwa ajili ya kufanikisha miradi mikubwa ya maji mkoani Njombe, Sh. bilioni 42 zitapelekwa Makambako, Sh. bilioni 50 Wanging'ombe na Sh. bilioni 29 mjini Njombe.

Kwenye elimu, Dk. Magufuli alisema serikali itaendelea kutoa huduma ya elimu bila malipo, kukamilisha ujenzi wa chuo cha ufundi stadi (VETA) ili vijana wa mkoa wa Njombe wapate mafunzo na ajira.



Kuhusu afya, Dk. Magufuli alisema serikali itakamilisha ujenzi wa hospitali ya rufani ya mkoa wa Njombe sambamba na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa nne itakayoelekea katika hospitali hiyo.

Alisema pia kutajengwa hospitali ya wilaya, vituo vya afya sambamba na kupatia vifaa vya upasuaji ili wananchi waweze kupata huduma ya upasuaji.

Serikali, alisema itanunua vichwa vya treni saba, kukarabati mabehewa 21, upanuzi wa bandari ya Manda iliyoko Ziwa Nyasa, vijiji 91 kufikiwa na umeme pamoja na kutatua changamoto ya tozo ya mazao wakati wa uvunaji inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

**MAFANIKIO NJOMBE**

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano, mkoa wa Njombe umepata mafanikio lukuki ikiwamo Sh. bilioni 498.76 kutumika katika ujenzi wa barabara.

"Nyakati za mvua baadhi ya barabara zilikuwa ni shida kupitika, kwa mfano barabara ya Ludewa-Makete-Njombe, wananchi walikuwa wanatumia siku mbili kusafiri, leo wanatumia saa chache," alisema Dk. Magufuli.

Alisema pia kumejengwa soko, stendi ya kisasa, Sh. bilioni 41.1 kutumika katika huduma ya afya, Sh. bilioni 44.108 zimetumika kuboresha na kupanua wigo wa elimu kati ya hizo Sh. bilioni 21 zilitumika kuhudumia elimu bure na Sh.bilioni 22.169 ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu.

"Miradi 84 ya maji imejengwa ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 24.58, vijiji 290 kati ya 381 vimefikiwa na huduma ya umeme," alisema.

**KIFO KADA UVCCM**

Wakati huohuo, Rais Magufuli aliviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Vyuo Vikuu mkoani Iringa, Emmanuel Mlelwa, wahusika na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Pia aliwataka wananchama wa CCM kuwa watulivu, kufanya kampeni kistaarabu, kutotumia lugha za matusi, kutojiingiza katika vurugu, bali wawaeleze Watanzania mambo ya maendeleo ya nchi.

# UPDP kuwakomesha wala rushwa tuzo viboko 100

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha UPDP, Ibrahim Twaribu Kadege, amesema ikiwa Watanzania watakipatia chama hicho ridhaa ya kuongoza nchi, serikali yake itapitisha bungeni muswada wa atakayebainika kuhusika na rushwa apewe tuzo ya kwenda gerezani miaka 100 na kupata viboko 100.

Kadege alisema hayo wakati akihutubia kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu mjini Morogoro uliofanyika katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema endapo UPDP itapata ridhaa ya kuongoza nchi, serikali yake itaimarisha zaidi mapambano dhidi ya rushwa kwa kuweka adhabu kali kisheria kwa watakaobainika kutoa ama kupokea rushwa.

Kadege alisema akiwa madarakani kazi yake ya kwanza atapeleka muswada bungeni na mapendekezo yatakayokuwa na maelekezo ya mtu yeyote akipatikana na hatia hiyo kuhakikisha anapata adhabu kikamilifu.

"Sisi tunapendekeza hivi atakayepatikana na kosa la rushwa kama kutoa au kupokea basi atapelekwa mahakamani na mahakama itatoa tuzo hatusemi adhabu sisi tunasema tuzo, na hii haitajali kuwa huyu ni mjomba, shangazi, mtoto wangu wala mpwa wangu, atapata viboko 100 na miaka 100 jela tuone kama mtu atakula rushwa," alisema.

Alisema kama chama chake kitapewa ridhaa ya kuongoza nchi kitaongeza kasi ya ujenzi wa barabara za lami vijijini na kununua ndege nyingi zaidi ili kuimarisha sekta ya usafiri na usafirishaji nchini.

Alisema wanakubali kuwa Rais John Magufuli amefanyakazi vizuri na wao kama chama watafanya vizuri zaidi na kama Magufuli aliweza kununua ndege 11, UPDP itanunua ndege zaidi ya 25.

"Tutaanzia kuweka barabara ya lami vijijini kwa kuwa kule ndio kuna uzalishaji wote wa vyakula hivyo hatuwezi kuacha kuboresha vijijini," alisema mgombea huyo.

Alisema mpango wa serikali ya UPDP unalenga kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo na uvuvi na kwamba endapo Watanzania watakipatia chama hicho ridhaa itawawezesha wananchi kuondokana na ukulima wa zamani uliopitwa na wakati.

Naibu Katibu Mkuu wa UPDP, Rajabu Hoza, akiomba kura kwa wananchi kwa mgombea urais alisema wakiwapa kura watahakikisha wanawapatia wananchi trekta ndogo na trekta kubwa na kuwawekea katika maeneo ya kilimo, ili kuondokana na tabu ya jembe la mkono na kuwapatia vifaa vya kulimia na kuvunia vya kisasa.

# Ataka Dk. Mengi aenziwe kwa Tuzo

**Na Christina Mwakangale, TANGA**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, ameshauri Baraza la Habari Tanzania (MCT) pamoja na wadau wa habari kuandaa tuzo itakayomuenzi hayati Dk. Reginald Mengi, kutokana na mchango wake kwenye tasnia ya habari.

Alisema Dk. Mengi alikuwa Mtanzania wa kwanza nchini kuwekeza katika tasnia hiyo, ikiwamo kuanzisha kampuni ya magazeti ya The Guardian Limited kituo cha Redio One pamoja na Televisheni (ITV).

Shigela aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati akitoa hotuba kwenye usiku wa Tuzo za Umahiri kwa Waandishi wa Habari Tanzania (EJAT), zinazoandaliwa na MCT. "Ni lazima tufikirie nini cha kufanya katika kumuenzi Dk. Mengi, amefanya mambo mengi makubwa katika tasnia hii, mchango wake hautasahaulika. Dk. Mengi, ni kati ya wawekezaji wa kwanza waliojitoa katika kuhabarisha tangu miaka ya 1990," alisema Shigela na kuongeza:

"Nimekuwa nikitafakari, na nilikuwa namheshimu mzee Mengi, nimekuwa nikitambua mchango wake, tutafakari, ndio kiongozi wa kwanza, mfanyabiashara aliyeamua kuwekeza katika habari. Magazeti, Mengi, Tv nazo Mengi, Redio, Mengi."

"Michango ya watu lazima tutafute namna ya kuappreciate (kushukuru) waliofanya makubwa, tusipotambua michango hii hata mlioanzisha tuzo hizi hamtakumbukwa."

Vile vile, Shigela alisema, mchango wao unatambulika zaidi katika vipindi maalumu hususan katika kipindi hiki cha uchaguzi mkuu na kwamba vyombo hivyo vimeripoti taarifa za wagombea wa vyama vyote bila upendeleo.

"Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, vyama vya siasa wagombea wanagombea kwa nafasi mbalimbali, vyombo vya habari vina nafasi kubwa, na safari hii nimefarijika sana ninapofuatilia habari kwa kiasi kikubwa wame-balance (kutendea haki)."

"Hauwezi ukaangalia kwenye kituo kimoja au ukasoma kwenye gazeti ukakuta ni habari ya mtu mmoja tu. Unaweza ukaangalia sera za wagombea wanne au watano utajifunza kupitia sera zao, kwamba ni chama gani au mgombea gani ana mwelekeo mzuri na kukichagua," alisema Shigela.

Pia, alisema kupitia vyombo vya habari vinavyotoa habari bila upendeleo, kumeendelea kufanya taifa kuwa na umoja. "Tungekuwa na vyombo vya habari vinavyochochea uchochezi, kufitinishana, sidhani kama taifa lingekuwa na umoja. Waasisi wa taifa letu Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume hadi sasa, Rais John Magufuli na Dk. Shein, vyombo vyetu vimeendelea kufanya vizuri."

Kadhalika, Shigela alisema vyombo vya habari vimekuwa ni chachu ya kuelimisha, kutoa burudani, fursa, kutatua changamoto na kuleta maendeleo.

"Kupitia vyombo hivi tunajifunza, tunaelimika na kufahamu namna ya kukabiliana na changamoto, ni platform (jukwaa) muhimu sana, inakufanya mtu ujue namna ya kujipanga hata inapotokea majanga, kama magonjwa ya corona tusingekuwa na vyombo hivi ingekuwa si rahisi, kwa kuwa baadhi wangetoa habari ambazo si sahihi," alieleza Shigela.

Alisema kupitia vyombo vya hababri ukweli unafahamika kwa kuufahamisha umma na serikali itaendelea kushirikiana, na vyombo hivyo pamoja na kuboresha mazingira ya kazi.

"Serikali imeendelea kuhakikisha taaluma ya habari inakuwa inayoheshimika na si ya kuchezewa, vyombo vya habari vinasaidia kutoa mawasiliano kati ya serikali na wananchi."

"Tusiwe waoga kuzungumza na vyombo hivi wala tusivione kama sehemu ya maadui, ukiangalia tuzo nyingi zilizoshindanishwa mwaka jana zimetuelezea sisi watu wa serikali, tuwe tunatoa ufafanuzi wa masuala yanayoibuliwa na waandishi kwenye kijamii," alifafanua Shigela.

Kuhusu tuzo hizo, Shigela alisema zinasaidia kutambua na kukubali mchango wa waandishi na kutoa hamasa na kwamba waliobuni tuzo hizo wanastahili pongezi.

HABARI KITAIFA

# NEC sasa yakunjua makucha wagombea matusi na kashfa

Na Waandishi Wetu

ZIKIWA zimesalia siku 29 kufanyika Uchaguzi Mkuu mwaka huu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewataka wagombea na vyama vya siasa kuzingatia maadili ya uchaguzi kwenye kampeni na kuepuka lugha za uchochezi zinazotishia usalama wa nchi.

Aidha, imewahakikishia Watanzania kuwa itasimamia uchaguzi huo kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu ili uwe huru na haki.

Akifungua jana mkutano wa tume hiyo na wadau wa uchaguzi mkoani hapa, Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mbarouk Salim Mbarouk, alisema wagombea kwenye kampeni zao wanapaswa kujiepusha na lugha za kashfa.

Jaji Mbarouk alisema kunapokuwa na malalamiko yoyote ya kimaadili, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao ikiwamo kuwasilisha malalamiko kwenye Kamati za Maadili ndani ya muda uliowekwa.

"Tunawakumbusha kipindi hiki sheria nyingine za nchi hazijasimama, hivyo wajihadhari na vitendo au matamshi ambayo yatasababisha vurugu kwa kisingizio cha uchaguzi," alisema.

Aliwahakikishia wadau kuwa tume hiyo itahakikisha uchaguzi mwaka huu unakuwa huru, wazi, haki na kuaminika kwa kuweka mazingira sawa ya ushindani kwa wagombea.

"Pia tunawatoa hofu wapigakura wenye mahitaji maalum kwa kuwa tumeshatoa maelekezo kwa watendaji kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu, wajawazito, akina mama wanaonyonyesha waliokwenda na watoto vituoni, wazee na wagonjwa," alisema.

Kadhalika, alisema kwa wasioona kila kituo cha kupigia kura kitakuwa na kifaa cha maandishi ya nukta nundu.

Akizungumzia kuhusu vifaa, makamu mwenyekiti huyo alisema NEC inaendelea na mchakato wa ununuzi wa vifaa na uchapishaji wa nyaraka na kwamba zabuni zote zimeshatangazwa na zinahusisha uchapishaji wa fomu mbalimbali.

Jaji huyo alisema tume inatarajia kuwa na vituo vya kupigia kura 80, 155 kati ya hivyo 79,670 vya Tanzania Bara na 485 Zanzibar na pia itatumia vituo 1,412 vya ZEC kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

"Kila kituo kati ya hivyo, kitakuwa na wapiga kura wasiozidi 500. Orodha ya vituo imewasilishwa kwa wasimamizi wa uchaguzi kwa ajili ya maandalizi na viongozi wa vyama vya siasa ngazi ya jimbo watapatiwa hiyo orodha siku 14 kabla ya siku ya uchaguzi ili kuwawezesha kuwasilisha orodha ya majina ya mawakala watakaopangwa kwenye vituo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Habari na Elimu ya Mpigakura, Giveness Aswile, alisema vifaa vingine vimeanza kupokelewa na karatasi za kura zitakuwa za mwisho kutolewa kutokana na mchakato wake kuwa mrefu.

Aidha, alisema kwenye vituo hivyo kutakuwa na watendaji 320,620 ambao watasimamia na kuendesha upigaji kura vituoni.

**WASIOONA WAKUMBUKWA**

TUME ya Taifa ya uchaguzi (NEC) imeandaa jalada la nukta nundu kwa kila kituo cha kupigia kura, kifaa ambacho kitawawezesha wapigakura wasioona na wenye uwezo wa kusoma maandishi ya nukta nundu .

Kifaa hicho pia kitatumika kwa wasioona watakaopenda kukitumia kupigia kura bila ya kuwa na wasaidizi.

Hayo yalisemwa jana na mwakilishi wa mkurugenzi wa NEC , Hamidu Mwanga, katika mkutano wa wadau wa uchaguzi uliofanyika Kibaha, mkoani Pwani.

Mwanga ambaye pia mkurugenzi wa NEC Zanzibar, alisema walemavu wana haki ya kupiga kura kama watu wengine.

"Kulikuwa na malalamiko miaka ya nyumba kutoka kwa wasioona ambapo wanapinga kura kwa kuomba msaada wa kupelekwa na hawajui wanayempigia ni yule anayemtaka au la," alisema.

Hamidu alisema tume imejianda ambapo imehakikisha shughuli zote za uchaguzi zinaenda vizuri.

Alisema idadi ya wapigakura waliojiandikisha ni 29,188,347 kwa ajili ya kumchagua raisi, wabunge na madiwani.

Aliongeza kuwa wanawake ni 14,691,743 ambapo ni sawa na asilimia 50.

Alisema wanaume ambao wstapiga kura wapo 14,494,604 sawa na asilimia 49 mbapo vijana wenye umri kati ya 28/35 ni 15,650,998.

Aliongeza kuwa vijana wa kiume 7,804,848 wa kike 7,846,153.

Alisema watu wenye ulemavu ambao watapiga kura ni 13,211 kati yao 2,223 ni walemavu wa macho, 4911 wana ulemavu wa mikono na 6,077 wana ulemavu wa aina nyingine.

Alisema tume itahakikisha uchaguzi wa mwaka huu unakuwahuru na wenye haki.

" Tumejipanga kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru nawa haki nawa uwazi," alisema.

Alisema tume itatumia vituo vya kupigia kura 80,155 katika uchaguzi mkuu mwezi ujao.

Aliongeza kuwa Kati ya vituo hivyo, Tanzania bara itakuwa na vituo 79,870 na Tanzania Zanzibar vituo 485.

Naye Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, aliwataka Watanzania kuepuka watu wanaotamani kuiona Tanzania ikiingia kwenye machafuko katika kipindi hiki cha uchaguzi

Aidha, Mtupa alitoa angalizo kwaTume kuhakikisha wanamtangaza mshindi mapema baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika.

Padri wa Kanisa la Katoliki, Benno Kikudo, aliwasihi wananchi kuhakikisha viongozi wanaowachagua ni wale watakaosimamia misingi ya amani na rasilimali za nchi.

Akiwakilisha mada katika mkutano huo Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura, Monica Mnanka alisema time inahakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki kama inavyotakiwa kwa mijibu wa ibara ya 5 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA, Yasmine Protace na Julieth Mkireri, KIBAHA

# Polisi yaonya wagombea, wafuasi

Na Augusta Njoji, DODOMA

JESHI la Polisi limetoa tamko kwa wagombea na wafuasi wao likiwataka kuacha kutoa lugha za matusi na kupandikiza chuki kwa wananchi

Pia, limewataka kufuata ratiba ya kampeni iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), huku likisema halitamuonea aibu mtu yeyote atakayekwenda kinyume cha sheria za nchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Liberatus Sabas, baadhi ya wagombea wamekuwa wakitoa lugha za matusi, uzushi na uongo, kashfa kwa wagombea wengine jambo ambalo ni kinyume na maadili na taratibu za uchaguzi.

Alikemea tabia ya wafuasi kuchana bendera na mabango ya wagombea wengine.

"Miongoni mwa matatizo yanayojitokeza ni pamoja na baadhi ya wagombea kutofuata ratiba ya kampeni iliyotolewa na Tume," alisema.

Alisema vyama vyote vinatakiwa kufuata ratiba na kama kuna chama kinataka kubadili ratiba kinatakiwa kuwasiliana na Mkurugenzi wa NEC.

"Kuna mgombea mmoja anafanya kwa makusudi kwenda kufanya mikutano sehemu ambayo hana ratiba ya kampeni, umuhimu wa kufuata ratiba ni kulifanya jeshi kutoa ulinzi kwenye hiyo mikutano, kwenda sehemu ambazo hayupo kwenye ratiba ni kujipeleka hatarini," alisema.

Alisema jeshi hilo lipo kwa ajili ya kuhakikisha kila mmoja anakuwa salama na kusisitiza kuwa watasimamia ratiba ya NEC na mgombea atafanya mkutano sehemu aliyoelekezwa.

"Tuliacha haya mambo yakawa yanaenda kienyeji kuanzia sasa tutaanza kuchukua hatua, maana tusipochukua hatua likitokea la kutokea sisi Jeshi la polisi ndio tutakaolaumiwa kwamba hatukutoa ulinzi ndio maana watu hawa wamezulika," alisema.

Kadhalika, alisema kuna wagombea baada ya kumaliza kampeni zao wanaamua kuingia mtaani kwa maandamano hadi usiku wakati ratiba inasomeka mwisho saa 12 jioni.

"Huko mtaani usiku usalama wako utakuwa hatarini na wakipata matatizo watakuja kulaumu Jeshi la Polisi, sasa nasema chama chochote chenye kampeni inapofika muda wa kumaliza kampeni watawanyike warudi nyumbani kwao, atakayekwenda kinyume na hapo tutachukua hatua," alisema.

"Kuna watu wanatoa vitisho kwa viongozi wa polisi na serikali, kila nchi inaongozwa kwa misingi ya kisheria, kanuni na taratibu zake, ambaye hatafuata tutamchukulia hatua bila kujali hayo anayosema," alisema Sabas. Aliwataka wananchi kutokubali kudanganywa kujiingiza kwenye vurugu na kuzipa tabu familia zao huku viongozi wao wakitanua mtaani.

"Jeshi la polisi lisingependa kutumia silaha wakati fedha zao ndio zimenunua, sisi ni sehemu ya familia tusingependa kupambana na wananchi ambao sisi ni sehemu yao, wananchi watii sheria bila shuruti ili nchi imalize uchaguzi kwa amani na utulivu,"alisema.





Polisi wakiusindikiza msafara wa mgombea mwenza wa urais kupitia CHADEMA, Salum Mwalimu, alipokuwa akiondoka Ifakara mjini, mkoani Morogoro jana. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# IPP Media yanyakua Tuzo 7 Umahiri wa Uandishi

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

WAANDISHI wa habari wa IPP Media, wameng'ara katika tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2019, kwa kuzoa tuzo saba, katika mashindano yaliyoshindanisha waandishi 56 kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini.

Walioshinda tuzo hizo kwa kushika nafasi za kwanza ni Sanula Athanas, Gwamaka Alipipi, Christina Mwakangale, Abdul Kingo na Rahma Suleiman (wote Nipashe), Crispin Gerald (The Guardian) na marehemu Agnes Almasy wa ITV.

Wengine walioshinda nafasi ya pili na ya tatu katika makundi mbalimbali ni Ashton Balaigwa (Nipashe- Morogoro), Marco Maduhu (Nipashe-Shinyanga) pamoja na Muhidini Msamba na James Kandoya wa The Guardian.

Awali, akizungumza katika utoaji wa tuzo hizo jijini hapa juzi, mmoja wa majaji katika shindano hilo, Pili Mtambalike, alisema ipo haja ya kuwaongezea uwezo waandishi wa habari katika kuandika habari za uchunguzi (IJ).

"Juhudi za ziada na wadau zinahitajika ili kuwajengea uwezo waandishi, sababu ndio inajenga sifa na umahiri wa chombo, IJ uandishi wake umepungua kwa kiasi kikubwa, japokuwa kuna changamoto katika 'media' nyingi," alisema Mtambalike.

Alisema katika mchakato wa kuwapata washindi, baadhi ya masuala jopo la majaji lilibaini changamoto ya kiuandishi, na kwamba lengo la tuzo hizo ni kutambua kazi zenye umahiri katika uandishi.

"Baadhi ya habari zilikuwa na vyanzo anuai. Vyanzo ambavyo vilitumika zaidi ni 'officialls' (wasemaji wa serikali) yaani RCs, wakuu wa wilaya, polisi lakini sauti za kijamii hazikupewa kipambele."

"Kuna umakini mdogo kwa baadhi ya waliowasilisha kazi zao, mfano walioleta CD hazikuwa na kitu yaani 'empty' inaonekana hawakuwa makini. Redio, televisheni na magazeti hazikuwa na 'back ground' (kueleza kilichotokea nyuma) inaonekana habari hizi hakuna uzingatiaji katika hili," alisema Mtambalike.

Kuhusu kazi za runinga, alisema mahojiano ya vipindi mazungumzo yalimpoka muongoza kipindi na kumuachia mgeni aliyealikwa studio kuongea muda mrefu.

Sanula ambaye ni Mhariri wa habari wa Nipashe, alishinda tuzo mbili katika kipengele cha mwandishi bora wa Habari za Utalii na Uhifadhi, Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora na kushika nafasi ya pili katika Habari za Elimu.

Pia Christina Mwakangale alishinda tuzo ya kipengele cha Habari za Jinsia na Afya ya Uzazi huku Gwamaka Alipipi akishinda, Habari za Athari za Kemikali kwa Afya na Binadamu na Mazingira.

Rahma Suleiman, alishinda mshindi wa kwanza tuzo ya mwandishi bora, Habari za Jinsia na kushika nafasi ya tatu kwenye kipengele cha Habari za Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Wengine ni Crispin Gerald, aliyeshinda tuzo ya Habari za Usalama Barabarani huku marehemu Agnes Almasy wa ITV, akishinda tuzo ya Habari za Madhara ya Kemikali kwa Afya na Mazingira kwa upande wa runinga.

Washindi wengine ni James Kandoya wa gazeti la The Guardian, aliyeshika nafasi ya tatu habari za usalama barabarani na Ashton Balaigwa (Nipashe), alishika nafasi ya pili kipengele cha Habari za Utalii na Uhifadhi.

Mchoraji wa Katuni Bora wa mwaka ni Abdul Kingo, aliyeshinda nafasi ya kwanza na ya pili, wakati Muhidini Msamba, akikamata nafasi ya tatu.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema tuzo hizo zimechelewa kutolewa mwaka huu kutokana na changamoto ya kifedha na janga la corona.

Alisema tuzo hizo ni za 11 tangu zilipoanzishwa mwaka 2009, na kwa mara ya kwanza zimetolewa nje ya Jiji la Dar es Salaam na kusisitiza kuwa utaratibu huo utaendelea miaka inayofuata.

"Mwaka huu tumetoa tuzo jijini Tanga, tuna imani miaka mingine zitafanyika kwenye mikoa mingine, na si tu Dar es Salaam kama ilivyozoeleka," alisema Mukajanga.

# Mtendaji asimamishwa tuhuma kufungia wanafunzi na nguruwe

**Na Gurian Adolf, NKASI**

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Said Mtanda, ameagiza kusimamishwa kazi Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Matala, Revocatus Tinga, kwa tuhuma za kuwafungia katika chumba kimoja wanafunzi na nguruwe waliokuwa wakizurura mitaani.

Akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Swahila, mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa, baada ya kupata taarifa hizo alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kumsimamisha kazi Ofisa Mtendaji huyo na kumpeleka mtendaji mwingine katika kijiji hicho.

Alisema kuwa, wanafunzi hao walifikishwa mbele ya mtendaji huyo wakituhumiwa kwa kosa la utoro shuleni na kabla ya kufikishwa kwake, wanafunzi hao walikuwa wamekamatwa na nguruwe wanao zurura mitaani na kuamuru wawekwe kwenye chumba kimoja na nguruwe hao.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa kitendo alichokifanya Ofisa mtendaji huyo hakikubaliki, hivyo inalazimu asimamishwe kazi na baada ya hapo akabidhiwe kwenye vyombo vya serikali kwa ajili ya uchunguzi.

Alisema baada ya uchunguzi kukamilika na ikibainika kuwa ni kweli amefanya kitendo hicho ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria na mamlaka yake ya nidhamu.

"Ni jambo lisilolokubalika kwa mtendaji wa kijiji ambaye ni mlinzi wa amani katika kijiji na anafanya kitendo hicho, sisi kama serikali ni lazima tuchukue hatua stahiki," alisema.

Mtanda aliwataka watendaji wa serikali wilayani humo, kuwa waangalifu wanapotekeleza majukumu yao na kuzingatia sheria kuliko kuongozwa na mihemko ya hasira kwa kuwa hali kama hiyo imekuwa ikisababisha madhara.

# Mbaroni tuhuma kumkata mkewe kiganja cha mkono

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MFANYAKAZI wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) jijini Dar es Salaam, Ombeni Alfayo, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumkata mke wake kiganja cha mkono wa kulia kwa sime kwa madai ya wivu wa kimapenzi.

Akizungumza kwa huzuni jana, akiwa Hospitali ya Selian, wilayani Arumeru mkoani Arusha, Veronica Kidemi (30) ambaye ni mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiranyi na Mkazi wa Kijiji cha Siwandeti, alisema amefanyiwa kitendo hicho na mume wake.

Alisema Alfayo amekuwa na tabia ya kumtukana matusi mazito mara kwa mara na kumpiga kwa kutumia vitu vyenye ncha kali, huku wakati mwingine akimnyang'anya watoto wao wawili waliowazaa.

Kidemi alisema Septemba 26, mwaka huu, alitoka kazini saa 11:00 jioni kwenda eneo la Mianzini jijini Arusha kutoa fedha za kununua mahitaji ya familia na baada ya hapo alikwenda nyumbani.

"Nilipoingia nyumbani kwangu mume wangu (Alfayo) nilimkuta ndani, aliponiona akaanza kunitukana, huku akinikata mapanga na katika harakati za kukwepa nilishtuka mkono wangu wa kulia, umekatwa ukiwa umening'inia," alisema huku akilia.

Alisema kabla ya tukio hilo, vikao mbalimbali vya kifamilia vimekuwa vikifanyika pamoja na viongozi wa dini lakini mara kwa mara amekuwa akipigwa na baada ya kipigo ananyang'anywa watoto .

"Mume wangu ana wivu sana na nimepata vipigo mara kwa mara na pia nimekuwa nikinyang'anywa watoto wangu. Ninachoomba serikali inaisaidie nipate watoto wangu. Amekuwa akinidhalilisha sana huyu mume ananinyima hata kuongea na ndugu zangu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alithibitisha kupokea taarifa za tukio hilo huku akisema Kidemi alijeruhiwa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali mikono yake miwili na mume wake Alfayo na kusababisha kiganja cha mkono wa kulia, kutengana na sehemu nyingine ya mkono.

Alisema uchunguzi unaendelea ili kubaini chanzo halisi cha tukio hilo, ingawa taarifa za awali zinadai kuwa ni wivu wa mapenzi na mtuhumiwa alitoroka baada ya kufanya tukio, lakini amekamatwa jijini Dar es Salaam.

"Mtuhumiwa amekamatwa, kwa taarifa tulizonazo wanafanya mpango wa kumsafirisha hadi hapa Arusha kwa ajili ya taratibu zingine za kumfikisha vyombo vya sheria," alisema.

Daktari wa mifupa katika hospitali hiyo, Robert Julius, alithibitisha kumpokea mgonjwa huyo na kusema kwa sasa anaendelea vizuri.

## TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TAARIFA KWA UMMA

**Dar es Salaam, 28 Septemba 2020.**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kukamilisha zoezi la kupokea, kuchambua na kuamua rufaa zote zilizowasilishwa na kupokelewa kutoka kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, Rufaa za Ubunge mpaka zoezi linakamilika zilikuwa zimefikia 165. Majibu ya rufaa hizo yameainishwa katika orodha ifuatayo-

### ORODHA YA WAGOMBEA UBUNGE AMBAO RUFAA ZAO HAZIKUFANIKIWA

| Na. | JINA | CHAMA | JIMBO |
|---|---|---|---|
| 1 | ALLY BAKARI KAMBI | CUF | KONDOA MJINI |
| 2 | ALLY SAID MSUYA | NCCR MAGEUZI | BABATI MJINI |
| 3 | AMINA ABDUL-RAHIMAN KANYAMA | CHADEMA | BAHI |
| 4 | ASKOFU MUSA SAMSON MLAWI | NCCR-MAGEUZI | DODOMA MJINI |
| 5 | ATHUMAN ALI ISIMBULA | CUF | BABATI MJINI |
| 6 | BAKAR HASSAN HAMAD | AAFP | KOJANI |
| 7 | CHRISTINA AIDAN CHINANGWA | CUF | MADABA |
| 8 | DKT. DAVID MCIWA MALLOLE | ACT WAZALENDO | DODOMA MJINI |
| 9 | FAKI ALI FAKI | NCCR-MAGEUZI | KOJANI |
| 10 | FELIX MARCUS | DP | DODOMA MJINI |
| 11 | FRANK GABRIEL LYMO | ADA-TADEA | BABATI MJINI |
| 12 | HAULE LAMBILEKI JAMES | CHADEMA | LUDEWA |
| 13 | IDRISA OMARI | NCCR MAGEUZI | MKOANI |
| 14 | JOHN LUCAS SICHULA | ACT WAZALENDO | KALAMBO |
| 15 | JUMA KOMBO HAMADI | ACT WAZALENDO | MICHEWENI |
| 16 | KENNEDY MOSES SMTOWE | CHADEMA | KALAMBO |
| 17 | KHAMIS MOH'D NASSOR | ACT WAZALENDO | KIJINI |
| 18 | KHAMIS MOHAMED KHAMIS | ACT WAZALENDO | MKOANI |
| 19 | KIHWELO FREDRICK MODESTUS | CHADEMA | MAFINGA MJINI |
| 20 | MAHAMI M. KISUGURU | SAU | KIGAMBONI |
| 21 | MARIAM SALUM KINAMBI | ACT WAZALENDO | SINGIDA MAGHARIBI |
| 22 | MATENI VICTOR SICHONE | NCCR MAGEUZI | KALAMBO |
| 23 | MATHAYO PHILIPO GEKUL | CHADEMA | BABATI VIJIJINI |
| 24 | MESHACK JEREMIAH OPORUKWA | NCCR MAGEUZI | MEATU |
| 25 | MSABAHA RAJABU | CUF | KILOSA |
| 26 | MTATUU WILSON JOSHUA | ACT WAZALENDO | BABATI MJINI |
| 27 | MUHAMMED AMOUR MUHAMMED | ACT WAZALENDO | BUMBWINI |
| 28 | MWANDI ROBERT ATHUMAN | NCCR MAGEUZI | RUNGWE |
| 29 | MZEE SALEH ABDALLAH | ACT WAZALENDO | WAWI |
| 30 | NDESAMBURO LUISESIA PHILEMON | CHADEMA | MOSHI VIJIJINI |
| 31 | NORBERT FLAVIAN MARANDU | CHADEMA | HANDENI VIJIJINI |
| 32 | SABAHI KHAMIS ABDULLAH | ACT WAZALENDO | PAJE |
| 33 | SALVATORY EMILIANUS SEGE | CHADEMA | KILOSA |
| 34 | STANLEY CHARLES SHOO | CHAUMMA | HAI |
| 35 | SUDI SWAIBU KATIKIRO | ACT WAZALENDO | KONDOA MJINI |
| 36 | SULEIMAN KHALFAN SAID | ACT WAZALENDO | OLE |
| 37 | TADEY LISTER MLEMETA | CHADEMA | BABATI MJINI |
| 38 | VEDASTUS SIMON MUNA | ACT WAZALENDO | SINGIDA MASHARIKI |
| 39 | MAGOZI MOHAMED ALLY MARJEBY | CUF | IGALULA |

### ORODHA YA WAGOMBEA UBUNGE AMBAO WAMEREJESHWA BAADA YA UAMUZI WA RUFAA

| Na. | JINA | CHAMA | JIMBO |
|---|---|---|---|
| 1 | ADEN BAHATI MAYALA | CHADEMA | SONGEA MJINI |
| 2 | ADO SHAIBU ADO | ACT WAZALENDO | TUNDURU KASKAZINI |
| 3 | ADOLF PELEUS MUKONO | CHADEMA | KARAGWE |
| 4 | AHMAD MOHAMED MKANGWA | NRA | ILEMELA |
| 5 | ALI OTHMAN ALI | CUF | WINGWI |
| 6 | ALLY SHANGWELI MBWAMBO | NCCR MAGEUZI | SAME MASHARIKI |
| 7 | AME IS-HAKA SHEHA | ACT - WAZALENDO | NUNGWI |
| 8 | ANNA ATHUMANI DAURI | ACT - WAZALENDO | SONGEA MJINI |
| 9 | ANNA DANIEL KAPINGA | ADA-TADEA | SONGEA MJINI |
| 10 | BASHIRI ALLY MUYA | CUF | HANDENI VIJINI |
| 11 | BONIFACE BONIFACE JACOB | CHADEMA | UBUNGO |
| 12 | BONIFASIA AIDAN MAPUNDA | ACT WAZALENDO | NAMTUMBO |
| 13 | CLEMENT PANCRAS PETER | DP | ILEMELA |
| 14 | DEVOTHA MATHEW MINJA | CHADEMA | MOROGORO MJINI |
| 15 | DISMAS ANDREA LUHWAGO | CHADEMA | WANGING'OMBE |
| 16 | DUNIA JUMA ALLY | ACT WAZALENDO | IGALULA |
| 17 | ERASTO KICHAMO TUMBO | NCCR MAGEUZI | ULANGA |
| 18 | FANUEL ELIAS MKISI | CHADEMA | VWAWA |
| 19 | HAMADI HAMADI KAMTANDE | CHADEMA | LIWALE |
| 20 | HAMISI ATHUMANI UREMBO | DP | KIGAMBONI |
| 21 | IDDI SALEHE KIZOTA | CHADEMA | KONDOA MJINI |
| 22 | JESCA DAVID KISHOA | CHADEMA | IRAMBA MAGHARIBI |
| 23 | JHIKOLABWINO SIZA MANYIKA | ACT WAZALENDO | NYASA |
| 24 | JOHARI JAMAL MLAGHANILE | NCCR - MAGEUZI | UBUNGO |
| 25 | JUMA HAJI SAUTI | CHADEMA | CHAANI |
| 26 | KHALIFA MUSA TENGEMEZA | NCCR MAGEUZI | SONGEA MJINI |
| 27 | KHAMIS ALI OMAR | ACT - WAZALENDO | TUMBE |
| 28 | KISESA STANSLAUS MICHAEL | ACT - WAZALENDO | MPANDA MJINI |
| 29 | KITALIKA EMANUEL TITHO | CHADEMA | MUFINDI KUSINI |
| 30 | KULUNGU HEMED RAMADHAN | CHADEMA | SINGIDA MAGHARIBI |
| 31 | KURWA NKWERA LUBUVA | CHADEMA | KIBITI |
| 32 | LUKUMAI EMANUEL MATAYO | CHADEMA | BAGAMOYO |
| 33 | LUKUZAZO LIBERATUS PASTORY | CHADEMA | BUHIGWE |
| 34 | LUMOLA STEVEN MAZIKU KAHUMBI | CHADEMA | BUKENE |
| 35 | MADOGA AISHA SALEHE MAULID | CHADEMA | DODOMA MJINI |
| 36 | MAEMBE VITALI MATHIAS | ACT WAZALENDO | BAGAMOYO |
| 37 | MAGERELI LUCY SIMON | CHADEMA | KIGAMBONI |
| 38 | MAMBO AHAMAD ARON | CUF | SONGEA MJINI |
| 39 | MAPAKO ABEID HAROUB | CUF | MOROGORO MJINI |
| 40 | MATUTURA ABDALLAH MATUTURA | ACT WAZALENDO | TUNDURU KUSINI |
| 41 | MGAWE ERNEST STANLEY | CHADEMA | KIBAMBA |
| 42 | MIRAJI MOHAMED HUSSEIN | CHADEMA | LUPA |
| 43 | MIZE ALI HAJI | CHADEMA | KIJINI |
| 44 | MNJEJA AYUBU MNJEJA | NCCR MAGEUZI | CHEMBA |
| 45 | MOHAMED JUMA MTAMBO | ACT - WAZALENDO | MKURANGA |
| 46 | MOHAMED SALUM KHALFANI | ACT WAZALENDO | TABORA KASKAZINI |
| 47 | MTUMWA HAJI MAKAME | ACT WAZALENDO | TUMBATU |
| 48 | MUSSA BAKARI MBAROUK | CUF | TANGA MJINI |
| 49 | MWASOTE JOSEPH MJENDA | CHADEMA | MBEYA VIJIJINI |
| 50 | NGULANGWA MOHAMED MSHAMU | CUF | BAGAMOYO |
| 51 | OMARY ALI OMARY | ACT WAZALENDO | WETE |
| 52 | OTHUMAN OMAR HAJI | ACT WAZALENDO | GANDO |
| 53 | PANDU HAJI SHEHA | NCCR-MAGEUZI | MKWAJUNI |
| 54 | PAUL LUCAS SOLEJI | NRA | NYAMAGANA |
| 55 | RAMADHANI ABDALLA RAMADHANI | ADA - TADEA | GANDO |
| 56 | REDDY JULIUS MAKUBA | ACT - WAZALENDO | TUNDUMA |
| 57 | REHEMA SWALEHE MJENGI | ADC | SINGIDA MASHARIKI |
| 58 | RENATUS PAMBA MKONGA | ACT WAZALENDO | UBUNGO |
| 59 | SALAMA OMAR MASOUD | CUF | KIGAMBONI |
| 60 | SEKELA GODFREY KAYUNI | ADC | KIGAMBONI |
| 61 | SHAIBU HUSSEIN SHESHE | ACT - WAZALENDO | MOROGORO MJINI |
| 62 | STEPHEN MERTUS HAMIS | CHADEMA | KAVUU |
| 63 | SUPEET KIMARARI OLEPURUKO | ACT - WAZALENDO | NGORONGORO |
| 64 | SUPHIAN JUMA NKUWI | ACT - WAZALENDO | SINGIDA MAGHARIBI |
| 65 | TANZILU HATIBU ISEMA | CUF | CHEMBA |
| 66 | YOSEPHER FERDINAND KOMBA | CHADEMA | MUHEZA |
| 67 | ZAMDA ABDALLAH NGONYANI | CHADEMA | NAMTUMBO |

### ORODHA YA WAGOMBEA UBUNGE WANAOENDELEA NA UTEUZI BAADA YA UAMUZI WA RUFAA

| JINA | CHAMA | JIMBO |
|---|---|---|
| ABDALLAH ALLY KABARA | CHAUMMA | ILALA |
| ABDIRAHIM ALI SLUM | NCCR MAGEUZI | KONDE |
| ALI OMAR ALI | CUF | TUMBE |
| AMINA ATHUMAN AHUNGU | SAU | ILALA |
| AMIR MOHAMED SHEKIONDO | CHADEMA | MLALO |
| CHAYA PIUS STEPHEN | CCM | MANYONI MASHARIKI |
| CHUMI COSATO DAVID | CCM | MAFINGA MJINI |
| CLINTON NICOLAS JOVIN | NCCR MAGEUZI | ILALA |
| DAMAS DANIEL NDUMBARO | CCM | SONGEA MJINI |
| DKT. MWIGULU NCHEMBA MADELU | CCM | IRAMBA MAGHARIBI |
| EMANUEL LAURENT MNKAI | ACT WAZALENDO | MLALO |
| ENG. MSONGWE GODFREY KASEKENYA | CCM | ILEJE |
| FRANCIS KISHABI MASANJA | CHADEMA | KISESA |
| HAFIDHI OMARI JAFAR | DEMOKRASIA MAKINI | CHAMBANI |
| HASHIM JUMA ISSAK | CHADEMA | ILALA |
| HUSSEIN JUMA ABDALLAH | ACT WAZALENDO | ILALA |
| IDDI KHATIB HAMAD | ACT WAZALENDO | MICHEWENI |
| ISSA SULTAN ISSA | CHADEMA | TUMBE |
| JOHNSTONE NERMES LUZIBUKYA | CHADEMA | MEATU |
| JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE | CCM | KALAMBO |
| JUMA HAMAD OMAR | CCM | OLE |
| JUMA HAMADI JUMA | NCCR MAGEUZI | MICHEWENI |
| KHADIJA ISSA SELEMAN | CUF | KONDOA |
| KHALIFA MOHAMED ISSA | ACT WAZALENDO | MTAMBWE |
| KHAMIS HAMAD KHAMIS | CHADEMA | WINGWI |
| KHAMIS KASSIM ALI | CCM | WAWI |
| KHAMIS OTHMAN HAJI | NCCR MAGEUZI | TUMBE |
| KHATIB SAID HAJI | ACT WAZALENDO | KONDE |
| KINGU ELIBARIKI EMMANUEL | CCM | SINGIDA MAGHARIBI |
| KOMBO RASHID ALI | ACT-WAZALENDO | KOJANI |
| KUNDI HAJI KOMBE | ACT WAZALENDO | CHAANI |
| MAINISHO ATHUMAN ITESI | CCK | ILALA |
| MAKAME MNYAA MBARAWA | CCM | MKOANI |
| MBWANA HAJI MBWANA | CUF | MICHEWENI |
| MGENI KHATIB YAHYA | CCM | MTAMBWE |
| MIRAJI JUMANNE MTATURU | CCM | SINGIDA MASHARIKI |
| MOHAMED SOLEIMAN SAID | CHADEMA | KONDE |
| MONICA YUSUPH SAFARI | CHADEMA | KONDOA |
| MUHAMED KHALFAN ISSA | ACT WAZALENDO | PANDANI |
| MWANA FA, HAMIS MOHAMED MWINJUMA | CCM | MUHEZA |
| MWANYIKA DEODATUS PHILIP | CCM | NJOMBE MJINI |
| NAMKOVERA IBRAHIM HASSAN | CHADEMA | MKURANGA |
| NASSIR MOHAMED JUNYA | AAFP | MKOANI |
| NDAKIDEMI PATRICK ALOIS | CCM | MOSHI VIJIJINI |
| NGASSA GANJA MBOJE | CHADEMA | IGUNGA |
| NJUKI SAID SALIM | ACT WAZALENDO | KONDOA |
| OBOTE ELIAS S. KIMAMBO | DP | MOSHI VIJIJINI |
| RASHID ABDALLA RASHID | CCM | KIWANI |
| RASHID MWINSHEHE MZANGE | CUF | ILALA |
| SALEH MOHAMED SALEH | ADC | TUMBE |
| SALIM ABDALLAH HEREZI | ACT WAZALENDO | MTAMBILE |
| SALIM MUSSA OMAR | CCM | GANDO |
| SAMWEL GIPSON KISSANGA | UDP | ILALA |
| SELEMAN MUSA MPENEKA | DEMOKRASIA MAKINI | ILALA |
| SHILOGILE JOSEPHAT CLEMENT | CHADEMA | MANONGA |
| SILLO DANIEL BARAN | CCM | BABATI VIJIJINI |
| SWALLE EDWIN ENOSY | CCM | LUPEMBE |
| TADAYO JOSEPH ANANIA | CCM | MWANGA |
| ULEGA ABDALLAH HAMIS | CCM | MKURANGA |

215920802

**Tangazo hili limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi**
**S.L.P 10923, Dar es salaam**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umuhimu wa wanawake kuwa viongozi iwe ajenda

UMUHIMU wa wanawake kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi umekuwa ni ajenda ambayo imeendelea kujadiliwa kwa kasi na makundi mengi ya jamii.

Hoja ya msingi inayoelezwa ni kuwa wanawake wanao uwezo mkubwa wa kuwa viongozi katika nafasi mbalimbali za kufanya uamuzi zikiwamo za ngazi za mitaa, udiwani, ubunge, uwakilishi, uwaziri na hata urais.

Kwamba wanawake wana uwezo sawa na wanaume, isipokuwa mfumo dume ndio unaochangia waonekane kuwa hawawezi kuwa viuongozi kama ilivyo kwa wanaume.

Hata hivyo, tumeshuhudia jitihada mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa na wanawake wenyewe za kupinga udhalilisha huo, na kwa hakika wamethibitisha kuwa wanafaa kuwa viongozi katika ngazi zote za kuchaguliwa na kuteuliwa.

Katika kuthibitisha hilo, idadi ya wanawake imekuwa ikiongezeka kila uchao katika uongozi kwenye serikali za mitaa kuanzia vijiji, vitongoji, mitaa, madiwani, wabunge na wawakilishi.

Vilevile, katika nafasi za kuteuliwa wanawake wameendelea kuchomoza kwa mfano, ngazi za makatibu tawala wa wilaya, mikoa, wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na mikoa, makatibu wakuu na mawaziri.

Hali hii inathibitisha kuwa mawazo mgando na yaliyopitwa na wakati ya kuwadhalilisha wanawake kuwa hawawezi kuwa viongozi, ni uongo na uzandiki, hivyo ni wakati mwafaka sasa kwa jamii yote ya Tanzania kuendeleza ajenda ya kutaka usawa kwenye nafasi za uongozi.

Kwa kuona umuhimu wa wanawake katika uongozi wa nchi yetu, Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini nchini imebainisha kuwa inaamini wanawake wakichaguliwa kwenye nafasi za uongozi watakuwa na fursa ya kutunga sera na kushiriki katika vyombo vya uamuzi, hivyo watakuwa chachu ya kuleta maendeleo na mapinduzi ya kiuchumi nchini.

Imebainisha kuwa zipo sababu nyingi zinazomkwamisha mwanamke katika nafasi ya uongozi na moja ya vikwazo kwake kupata uongozi ni uwapo wa mfumo dume ndani ya vyama vya siasa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Sheikh Alhad Salum, wakati akizungumza kwenye warsha ya siku moja kuhusu nafasi ya mwanamke kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu katika mustakabali wa haki, heshima, amani na utulivu kuchagua viongozi bora.

Sheikh Salum ambaye pia ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema kuwa wanawake ni zaidi ya nusu ya idadi ya watu duniani, hivyo ili kutokomesha umasikini, lazima wanawake wapewe nafasi kikamilifu. Alitolea mfano kwamba Biblia ambayo inasema'wanawake watangazao habari ni jeshi kubwa(zaburi 68:11b), hivyo alisema ni wazi wanayo nguvu ya kufanikisha hili.

Alisema vyama vingi vya siasa vinawatumia wanawake katika shughuli za uhamasishaji, kuongeza idadi ya wanachama na kueneza sera za vyama hivyo, ikiwamo wakati wa kampeni katika kuwavutia wapigakura, lakini kwa asilimia kubwa hawawatumii kama wadau kwa kuruhusu wapewe nafasi za uongozi zenye nguvu ya maamuzi.

Kwa kuwa Katiba ya Tanzania imeweka wazi kwamba wagombea wa nafasi za uongozi wa siasa lazima watokane na vyama vya siasa, sisi tunaona kuwa vyama vya siasa vina jukumu na wajibu wa kuhakikisha kwamba vinatoa kipaumbele kwa wanawake kwa kuwapa fursa ya kuwania uongozi wa kuchaguliwa.

Vyama vya siasa vikiweka taratibu nzuri, uwazi, usawa na haki katika kutoa nafasi za kuwania uongozi, ni imani yetu kuwa wanawake wengi watapata fursa ya kushiriki katika kufanya uamuzi mbalimbali na kutunga sera zitakazoileta maendeleo nchi yetu na kuwanufaisha jinsi zote. Tunalipa msisitizo suala hili kwa kuwa wanawake wamekuwa wakikumbana na vikwazo vingi ndani ya vyama vya siasa, ukiwamo upendeleo na rushwa ya ngono katika kupata uongozi wa ndani ya vyama vyenyewe na wa kuwania uteuzi wa kugombea nafasi za dola.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wagombea ajenda ziwe za amani si chokochoko

LEO zinatimia siku ya 36 tangu kuanza kampeni za uchaguzi mkuu, ambazo pazia lake lilifunguliwa Agosti 26 pale wagombea walipoanza kunadi ilani na sera za vyama vyao kwa wapigakura.

Kwa hiyo baada ya ngwe ya kwanza zinasalia siku 27 za kampeni hizo ambazo zitahitimishwa mwezi ujao Oktoba 27 na kufuatiwa na uchaguzi utakaofanyika Jumatano Oktoba 28 .

Hata hivyo, wakati wagombea wa nafasi hizo wanaendelea kujinadi katika maeneo mbalimbali wapo baadhi wanasuasua kutokana na sababu mbalimbali ukiwamo ukata.

Katika mchakato huo wapo baadhi ya wagombea ambao wanakaririwa na vyombo vya habari wakitamka maneno, ambayo hana staha wakati wakielezea yale yaliyomo kwenye ilani za vyama vyao.

Kauli kwamba hakitaelewe- ka na mambo mengine yanayofanana na hayo, yanaweza kuwatisha wapigakura wakaogopa kujitokeza katika uchaguzi, hivyo suala la kuwa makini na kujikita katika ilani ni la muhimu.

Ikumbukwe kuwa katika idadi ya Watanzania ambao ni zaidi ya milioni 50, wapo wanachama wa vyama mbalimbali vya siasa na wengine si wanachama, lakini huwa wanashiriki katika uchaguzi. Sasa inapotokea baadhi ya wagombea wakitoa kauli tata, zinaweza kusababisha kuwanyima kura, kutokana na kwamba watu wataogopa kujitokeza siku ya uchaguzi na wengine watapigakura kwingine.

Ushawishi wa kupigiwa kura umo ndani ya ilani na sera, ambazo wananchi wanatakiwa kuambiwa wapate nafasi ya kuzichambua na kisha kuamua kama wameridhika nazo ama hawazitaki.

Uamuzi huo unakuwa ndani ya sanduku la kura ambalo ndilo lenye majibu, hivyo mgombea akienda kinyume na hayo, basi iwe na kufurahisha lakini ambayo yanawaogopesha hata wapigakura.

Wakati huu ambao zimebakia siku 27 za kampeni, wagombea wote hawana budi kuliona hilo na kulifanyia kazi kwa ajili ya kupata ushindi, lakini kikubwa zaidi ni kuhimiza ulinzi wa amani iliyopo ili iendelee kudumu.

Vilevile huu ndiyo wakati kwa wapigakura kuwapima wagombea kuanzia ngazi ya urais, ubunge na udiwani, ili hatimaye kupata viongozi watakaoshika nafasi hizo hadi mwaka 2025.

Wapigakura wasiwe watu wa kushabikia na kushangilia maneno ya wagombea bila kuyachambua, vinginevyo wanaweza wakachagua viongozi wasiowahitaji upo na kujikuta baadaye wakijuta.

Hivyo wasitawaliwe na mihemko ya kisiasa ama kushabikia hata mambo yasiyofaa wakati huu wa kampeni, bali wawe ni watu wa kuhoji ahadi za wagombea ili waambie ni jinsi gani zitatekelezwa.

Kwa mfano, katika ilani za vyama vya siasa zinaelezea kuboresha huduma mbalimbali za jamii zikiwamo za afya, maji na nyingine nyingi, hivyo ni nafasi adimu kwa wapigakura kuhoji ni jinsi gani zitaboreshwa.

Haitoshi mgombea kusema kwamba, akichaguliwa ataboresha huduma za afya, halafu wananchi wanashangilia bila kuhoji ni namna gani zitaboreshwa halafu siku ya kupiga kura wanamchagua.

Wagombea waulizwe maswali na watoe majibu yenye ufafanuzi wa kutosha kuliko kile ambacho ilani zimeeleza kwa kifupi, hali ambayo inasababisha watu kutofahamu kwa kina mikakati ya chama husika.

Hivyo wakati wanasiasa wakizingatia yaliyomo kwenye ilani za vyama vyao, wapigakura nao wanatakiwa kuhoji ili hatimaye wawe na uchaguzi sahihi wa viongozi wanaowataka.

Wasiwe tayari kukubali kuburuzwa na wanasiasa, ambao kauli zao zinaweza kusababisha umoja wa Watanzania ukawa mashakani, badala yake watumie kampeni zinazoendelea, kuwasoma na kuwachuja.

Si vibaya kuwa na kaulimbiu ya 'Tanzania kwanza mengine baadaye' ikiwa ni maalum kwa kuhamasisha amani na utulivu uliopo viendelee kudumu, kwa kutambua kwamba, kuna maisha baada ya uchaguzi.

# Mvua yabomoa nyumba, yajeruhi

Na Gurian Adolf, NKASI

WATU 11 wamejeruhiwa na nyumba 17 zimebomoka kufuatia mvua kubwa iliyoambatana na upepo katika Kijiji cha China Kata ya Kate wilayani Nkasi mkoani Rukwa na kuwaacha baadhi ya wakazi bila makazi.

Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, aliyetembelea kijiji hicho kujionea maafa hayo, ofisa mtendaji wa kijiji hicho, Conrad Kauzeni, alisema kuwa mvua hiyo ilianza kunyesha juzi saa 11 jioni, na baada ya muda ilinyesha tena huku ikiambatana na upepo mkali na kubomoa nyumba na watu 11 kujeruhiwa.

Alisema kuwa kufuatia hali hiyo, wananchi walijitokeza kuwaokoa wenzao, huku majeruhi wakikimbizwa kwenye Kituo cha Afya Kate kwa ajili ya matibabu.

Ofisa mtendaji huyo alisema wanamshukuru mwekezaji wa shamba la Msipazi Farm kijijini humo, Salum Sumry, kwa kutoa gari na kuwakimbiza majeruhi kituo cha afya pamoja na kugharamia matibabu ya waathirika hao.

Alisema mwekezaji huyo pia alitoa gunia 18 za mahindi kuwasaidia waathirika hao ili kupata chakula kipindi hiki kigumu.

DC Mtanda aliwataka wananchi kuwa watulivu katika kipindi hiki, huku akipongeza namna ambavyo wanavyoshirikiana kwa kusaidiana.

Alisema serikali itafanya tathmini ya maafa hayo kupitia kamati ya maafa ya wilaya, na kuwa baada ya hapo ndipo watajua kiwango cha uharibifu na serikali ijue wapi itasaidia.

**Akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, aliyetembelea kijiji hicho kujionea maafa hayo, ofisa mtendaji wa kijiji hicho, Conrad Kauzeni, alisema kuwa mvua hiyo ilianza kunyesha juzi saa 11 jioni, na baada ya muda ilinyesha tena huku ikiambatana na upepo mkali na kubomoa nyumba na watu 11 kujeruhiwa.**

# JKCI kuwapima wagonjwa moyo bure wakazi wa Dar

Na Joseph Mwendapole

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), inatarajia kuwapima magonjwa ya moyo bure wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani katika maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano JKCI, Anna Nkinda, upimaji huo ambao umeanza leo jijini hapa, utafanyika na utoaji wa elimu ya lishe bora kwa afya bora ya moyo.

Ilisema upimaji utafanyika katika viwanja vya Tanganyika Packers vilivyopo Kawe, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam kwa kufanya upimaji kwa watoto na watu wazima.

Taarifa hiyo ilisema wananchi watapimwa urefu, uzito, shinikizo la damu (BP), sukari na kupewa ushauri wa kitaalamu wa kuepuka maradhi hayo.

"Kwa wale watakaokutwa na matatizo ya moyo watafanyiwa uchunguzi zaidi na kupatiwa matibabu na kaulimbiu yetu ni maamuzi sahihi kwa afya bora ya moyo," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema wafanyakazi wa JKCI watahakikisha wanatoa huduma bora zaidi za magonjwa ya moyo kwa wananchi wenye matatizo hayo.

"Mpango wetu ni kutoa tiba ya moyo, upasuaji wa moyo na elimu kwa jamii, ambayo itawasaidia wananchi kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu magonjwa hayo, ambayo ni moja ya yasiyoambukiza na mtu anaweza kuyaepuka kwa kufuata ushauri wa kitaalamu," alisema.

Aliwaomba wananchi waadhimishe siku hiyo, kwa kujitokeza kwa wingi kupima afya zao, ili kujua kama wana matatizo ya moyo au la, hivyo kuanza matibabu mapema kwa kuwa asilimia kubwa ya wagonjwa wanaopokelewa JKCI, wanakuwa katika hali mbaya.



Waendesha guta wakiwa wamesheheni mzigo wa magodoro na kuwafanya washindwe kuona nyuma katika eneo la Viwandani Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mhagama atamba ujenzi viwanda zaidi ya 8,000

Na Richard Makore, MWANZA

SERIKALI imesema kati ya mwaka 2015 hadi mwaka 2019, viwanda 8,477 vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali ya nchi vikiwamo vikubwa, kati, vidogo na vidogo zaidi.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, alipofungua mkutano wa wadau na bidhaa za ngozi.

Waziri Mhagama alisema, bidhaa za ngozi ni muhimu kwa ajili ya kiwanda kikubwa ambacho wameingia ubia kati ya Jeshi la Magereza nchini na Mfuko wa Mafao kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Alisema dhana ya ujenzi wa viwanda hapa nchini imesaidia kuzalisha ajira kwa vijana nchini, huku kundi hilo likichukua asilimia 56 ya nguvu kazi.

Mhagama alisema ikiwa juhudi za kuongeza viwanda zitafanyika kuna uwezekano wa kuongeza ajira na kwamba asilimia 8.5 ya pato la taifa linatokana na sekta hiyo nchini.

Aliitaka mifuko ya hifadhi kuwekeza kwa faida badala ya kukaa na fedha za wanachama wanazopokea kila mwezi.

"Huwezi kukaa na fedha za wanachama bali ziwekezwe katika miradi ambayo ni endelevu ambayo inatoa faida," alisema.

Alisema bidhaa za ngozi zinatarajia kupata soko kupitia kiwanda cha ngozi cha Kilimanjaro na kinazalisha viatu, mikoba ya wanawake, mikanda pamoja na bidhaa zingine ambazo zinatarajia kuuzwa ndani na nje ya nchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, akizungumzia uwekezaji huo, alisema ili kupata ngozi yenye ubora wametoa mafunzo kwa wachunaji 775 nchi nzima.

Vilevile, wameanzisha kampeni ya kutoa dawa za kuogeshea mifugo katika mikoa 20 ya wafugaji ili kupata ngozi yenye ubora itafaa katika viwanda.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa PSSF, Hosea Kashimba, alisema, kiwanda hicho kinamilikiwa kwa pamoja kati yao na Jeshi la Magereza.

Alisema PSSF inamiliki asilimia 86 na Magereza 14 na kwamba Watanzania 7,000 wanatarajia kupata ajira na kwamba wanatarajia kuzalisha viatu milioni 2.4.

Aliwataka wafugaji kutumia fursa hiyo kuzalisha mifugo yenye ubora ili kuwauzia ngozi na matarajia yao ni kuona Watanzania wengi wanatumia bidhaa za ndani zenye ubora.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
30 – 09 - 2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATANO tarehe 30/09/2020** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo yake yenye vipimo vikubwa. Kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili namba za usajili: **T176 DFN/ T171 DFN**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | **18.00** |
| **Upana** | - | mita | **2.84** |
| **Kimo** | - | mita | **5.20** |

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA hadi DAR ES SALAAM kupitia MOROGORO** Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115923002

## Aomba wananchi wakopeshwe matibabu

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MGOMBEA ubunge kwa tiketi ya CCM, Jimbo la Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, ameiomba serikali kufanya utaratibu wa mabadiliko katika sekta ya afya, ili wananchi waweze kupatiwa matibabu kwa kuwakopesha na kulipa gharama hizo mwisho wa mwezi.

"Kwa kweli kila mtu anahitaji matibabu, lakini kuna wananchi wengine hawana fedha za kulipa papo kwa papo ni bora kama serikali ingeona umuhimu wa kuwafanya kulipa mwisho wa mwezi kama ilivyo kwa bili nyingine," alisema.

Kishimba alitoa ombi hilo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni za udiwani katika Kata ya Nyihogo, Jimbo la Kahama Mjini, ambazo zililenga kumnadi mgombea udiwani wa kata hiyo, William Sindano.

Kishimba alisema hoja hiyo aliwahi kuizungumzia bungeni katika kipindi kilichopita na kuongeza kuwa Watanzania sio wote wanahimili gharama za matibabu kwa wakati huo huo.

"Tunaomba wananchi kama itawezekana wakopeshwe matibabu kama ilivyo kwa wateja wa bili za maji, ili waweze kulipa fedha hizo hata mwisho wa mwezi, ili kuwapunguzia adha ya kutafuta fedha kwa wakati huo huo wakati hawana," alisema Kishimba.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga aliyeshiriki katika ufunguzi wa kampeni hizo na kuwa mgeni rasmi alisema kuwa CCM, imetekeleza mengi katika kipindi kilichopita na kuongeza kuwa kama wananchi watakipa ridhaa tena watatatuliwa changamoto zao.

## NBC kinara maonyesho ya madini

**Na Mwandishi WETU,** GEITA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeibuka kinara kwenye Maonyesho ya Madini na Teknolojia yaliyomalizika mwishoni mwa wiki mkoani Geita.

Taasisi hiyo imefanikiwa kutwaa jumla ya tuzo tatu ikiwamo tuzo ya mshindi wa kwanza kwa taasisi za kifedha na benki zilizoshiriki kwenye maonyesho hayo. Benki hiyo pia ilifanikiwa kutwaa tuzo ya Mdhamini Mkuu wa maonyesho hayo kwa taasisi za fedha, huku pia ikifanikiwa kuibuka mshindi wa tatu wa jumla katika maonyesho hayo.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hizo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, aliyemwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Mkurugenzi wa Idara ya wateja binafsi, benki ya NBC Makao Makuu, Elibariki Masuke, alisema tuzo hizo tatu zinaakisi mafanikio makubwa ambayo benki hiyo imeyapata kupitia maonyesho hayo.

Aliongeza kuwa mkakati wa benki hiyo baada ya maonyesho hayo ni kutekeleza kwa vitendo masuala muhimu iliyoahidi kuyafanya kwa kushirikiana na wadau hao ili kuboresha zaidi sekta hiyo.

Aidha, kupitia makongamano mbalimbali benki hiyo iliwawezesha wadau wa sekta ya madini kubadilishana mawazo baina yao pia baina yao na mamlaka mbalimbali za serikali ikiwamo Wizara ya Madini, TRA, NEMC, SIDO na TANTRADE, TABWA, OSHA, GST na NSSF.

# Zaidi ya kaya 1,000 zaomba kujiondoa TASAF

**Na Ahmed Makongo,** MWANZA

JUMLA ya walengwa 1,320 wa mpango wa kunusuru kaya maskini mkoani hapa, wameomba kujiondoa baada ya maisha yao kubadilika na kumudu kujitegemea.

**Baada ya kikao hiki mtumie fursa hii mwende kuelimisha wananchi kwa kuandika habari sahihi.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Ladslaus Mwamanga, aliyasema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha kuwajengea uelewa waandishi wa habari wa mikoa minne ya Kanda ya Ziwa.

Kikao kazi hicho, kimeshirikisha wanahabari kutoka mikoa ya Kagera, Mara, Simiyu na Mwanza, kwa ajili ya kuwajengea uelewa kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF.

Mwamanga alisema kuwa TASAF imefanya kazi kubwa ya kuwabadilisha walengwa kutoka kwenye umaskini uliokithiri na kuingia umaskini wa kati na tayari baadhi ya walengwa nchini wameondokana na umaskini.

"TASAF imefanya mambo makubwa sana kwa kunusuru kaya maskini, baadhi ya walengwa wameondokana na umaskini uliokithiri na pia baadhi yao wamechaguliwa kuwa viongozi, wengine wamekuwa wenyeviti wa vijiji kwa sababu kwa sasa wana hali nzuri kimaisha," alisema.

Akifungua kikao kazi hicho, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Tutuba, alisema kuwa kupitia mafunzo hayo, wanahabari wataisaidia TASAF kufahamika kwa wananchi kwa shughuli inazozifanya kuzikwamua kiuchumi kaya maskini.

"Baada ya kikao hiki mtumie fursa hii mwende kuelimisha wananchi kwa kuandika habari sahihi, maana nyinyi ni watu muhimu sana katika masuala ya maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla," alisema.

Aliwataka wanahabari kufuatilia wanufaika wa mpango huo na kuandika jinsi walivyonufaika na mpango huo.



Dereva wa bodaboda akiwa amepakia abiria mwenye mzigo kichwani pamoja na mizigo mingine katika eneo la Mbezi kwa Yusuf, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ofisa elimu awataka wahitimu sekondari kutamani vyuo vikuu

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WAHITIMU wametakiwa kutobweteka na elimu ya kidato cha nne waliyoipata, badala yake wanatakiwa kuendelea kusoma ya vyuo vya elimu ya juu.

Hayo yalisemwa na Ofisa Elimu taaluma Mkoa wa Pwani, Hildegard Makundi, katika mahafali ya 13 ya Shule ya Sekondari Victory, iliyopo Mkuranga mkoani Pwani.

"Baadhi ya wanafunzi wanapomaliza kidato cha nne, wanaona hapo ndio mwisho wa safari yao ya kimasomo, hivyo kuishia hapo haitakiwi, inatakiwa kufika mpaka vyuo vya juu," alisema.

Aliongeza kuwa wapo ambao hawafanyi vizuri katika masomo yao, lakini wanajiendeleza na kufika vyuo vya juu.

Akizungumzia ujasiriamali wakutengeneza mafuta, kupika, picha na kutengeneza sabuni, ambao wameupata shuleni hapo, alisema ni wakati mwafaka umefika wanafunzi kujiingizia kipato pale wanapokuwa majumbani wakisubiri matokeo.

Alisema Shule ya Victory imefanya jambo zuri kwa kuwafundisha ujasiriamali wanafunzi na hali hiyo itawasaidia kujiongezea kipato.

"Uongozi wa shule mmefanya jambo zuri kwa kuwafundisha ujasiriamali wanafunzi, hivyo tutarajie mwendapo majumbani mtaendelea kutumia mafunzo ya ujasiriamali mliyoyapata kwa kujiongezea mitaji na hamtakaa vijiweni," alisema.

Pia, aliipongeza shule hiyo kwa kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, ambapo kwa sasa ni muhimu kutokana na Tanzania kuwa ya viwanda.

Alisema masomo ya sayansi yatasaidia kupatikana kwa idadi kubwa ya wataalamu katika sekta ya viwanda.

Kwa mujibu wa mwalimu mkuu wa shule hiyo, Ponsiano Mlelwa, zaidi ya wanafunzi 100, wanatarajia kuhitimu kidato cha nne mwaka huu.

Alisema, maadili na nidhamu vimeleta mafanikio makubwa katika shule yao, ambapo kwa miaka mitatu iliyopita, shule imeweza kufanya vizuri katika mitihani ya taifa ya kidato cha nne.

# Kamusi ya lugha ya alama kidijitali yazinduliwa

Na Mwandishi wetu

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imezindua kamusi ya kwanza ya lugha ya alama ya kidijitali, yenye lengo la kupunguza tatizo la mawasiliano katika ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi viziwi.

Akizindua kamusi hiyo mkoani Tabora, katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya viziwi yenye kaulimbiu "Kuhakikisha upatikanaji wa haki za binadamu kwa viziwi", Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Ave Maria Semakafu, alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa makundi yote yenye ulemavu kupata elimu na huduma nyingine za kijamii.

Dk. Semakafu alisema pamoja na maboresho makubwa yaliyofanyika katika sekta ya elimu, kundi la viziwi lilikuwa limeachwa nyuma huku tatizo kubwa likiwa ni mawasiliano na kutokuwapo kwa walimu wa kutosha, hasa katika ngazi ya sekondari.

**kutokana na hali hiyo serikali imeandaa kamusi hiyo, ili kuwa na lugha moja ya alama na kutoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha katika shule zinazopokea watoto viziwi.**

Alisema kutokana na hali hiyo serikali imeandaa kamusi hiyo, ili kuwa na lugha moja ya alama na kutoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha katika shule zinazopokea watoto viziwi.

"Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na lugha moja ya alama kwa ajili ya kuwezesha mawasiliano ya watumiaji wa lugha hiyo, hivyo itaendelea kusimamia uendelezaji na usanifishaji wa lugha ya alama, ili kuwezesha utoaji elimu kurahisisha ujifunzaji na kuboresha mawasiliano katika jamii," alisema.

Naye, Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, alisema kamusi hiyo ya lugha ya alama ya kwanza nchini imezinduliwa pia na mwongozo wa utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari kwa wanafunzi viziwi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba, alisema taasisi hiyo ilipewa jukumu la kuandaa Kamusi hiyo na wamefuata taratibu zote kwa kushirikisha wadau wote.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Elimu Maalum kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magret Matonya, alisema wizara imeanza ujenzi wa shule ya mfano ya viziwi katika Halmashauri ya Masasi, mkoani Mtwara ikiwa ni jitihada za kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji wanafunzi viziwi, ambao ujenzi wake utagharimu Sh. bilioni 1.5.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Taifa (CHAVITA), Selina Mlemba, aliishukuru serikali kwa hatua hiyo na kuwa miaka michache ijayo wanaamini watapata wataalamu wengi katika maeneo mbalimbali wakiwamo madaktari kwa kuwa sasa wamepata kamusi itakayowawezesha kusoma bila kikwazo.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tusiime ya jijini Dar es Salaam, wakitoa maelezo kwa Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa wateja wadogo na wa kati wa benki ya NBC, Mussa Mwindaho (wa pili kushoto), alipotembelea banda lao kwenye mahafali ya 16 ya shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau waipongeza NMB ahueni corona

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI na wadau mbalimbali wameipongeza Benki ya NMB kwa msaada wake mkubwa wakulisaidia taifa na wateja wake kukabiliana na changamoto za janga la corona ambalo athari zake kiuchumi na kibiashara zinaendelea kuitikisa dunia.

Pongezi hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Arusha wakati wa hafla ya mtandao wa wateja wakubwa wa benki hiyo wa Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa mitatu ikiwamo pia Tanga na Kilimanjaro.

Benki hiyo ilitangaza unafuu wa ulipaji mikopo kwa wateja wake Mei mwaka huu kupitia likizo ya marejesho ya mikopo yao na wengine wakiongezewa muda wa kulipa mikopo hiyo, ili kuwasaidia kukabiliana na madhara yaliyoletwa na COVID-19 katika biashara zao.

Wateja waliohudhuria hafla hiyo walisema ahueni hiyo imesaidia kuzinusuru biashara nyingi zisiteteleke sana au kufa kabisa. Kwa upande wake, uongozi wa serikali mkoani Arusha ulisema inastahili pongezi kwa kuwajali wateja wake kwa hali na mali wakati wa kipindi hiki kigumu.

"Iliwasaidia sana wateja wake na imeendelea kuwa nao karibu wakati wote wa kipindi hiki kigumu. Sisi kama serikali tunawapongeza kwa hilo. Ni jambo kubwa hasa kwa sekta ya utalii ambayo imeathiriwa sana na corona," Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha katika hafla hiyo, alisema.

Pia aliipongeza benki hiyo kwa utaratibu wake wa kukutana na wateja jambo ambalo alisema linasaidia kuboresha huduma zake na kuwahudumia Watanzania kwa ufanisi mkubwa. Mwaisumbe aliongeza kuwa benki hiyo imekuwa na jadi ya kushirikiana na serikali katika shughuli za kiuchumi na kijamii na ni mfano mzuri wa taasisi zinazobadilika kutokana na mazingira na mahitaji yaliyopo.

Akiongea katika hafla hiyo iliyowajumuisha zaidi ya wafanyabiashara wakubwa 100 wa Arusha na mikoa ya jirani, Ofisa Mkuu wa Huduma Jumuishi wa benki hiyo, Nenyuata Mejooli, alisema walitoa ahueni ya aina mbili kuwasaidia wateja kukabiliana na changamoto za corona.

Alifafanua kuwa nafuu hiyo iliyotolewa kutokana na mahitaji ya wateja ili kuhakikisha shughuli zao zinastahimili misukosuko ya COVID-19 ilikuwa ya kifedha na pia kubadilisha mfumo wa urudishaji mikopo kulingana na ukubwa wa athari.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, Alex Mgeni, msimamo wa Serikali ya Rais Dk. John Magufuli kuhusu corona umesaidia sana kupunguza hofu na athari za janga hilo nchini.

## 'CCM haiwezi kuteteleka makada kuhama'

Na Neema Sawaka, KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Shinyanga, kimesema licha ya kukimbiwa na baadhi ya wanachama kwenda vyama vingine vya siasa baada ya kushindwa katika kura za maoni, bado hakiwezi kuteteleka.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, wakati wa ufunguzi wa kampeni za udiwani katika kata ya Malunga iliyopo Halmashauri ya Mji wa Kahama Jimbo la Kahama Mjini.

Mlolwa alisema kuwa CCM inataka wanachama ambao ni wavumilivu wa kila kitu siyo wale wanaohama kwenda katika vyama vingine.

"Hata mimi nilishawahi kugombea katika nafasi mbalimbali ndani ya chama kwa zaidi ya mara tatu, lakini nilikuwa nikishindwa na sikuweza kujaribu kwenda chama kingine kabisa katika kipindi hicho hadi nilipopata uenyekiti wa Mkoa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa CCM kupitia ilani yake imefanikiwa kutatua matatizo mbalimbali yaliyokuwa yakiwakumba wananchi ikiwamo usambazaji wa umeme vijijini.

Kwa upande wake, mgombea udiwani katika Kata ya Malunga kupitia chama hicho, Joseph Mipawa, alisema ikiwa wananchi wa kata hiyo watampa ridhaa ya kuwaongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo atahakikisha anatatua changamoto zinazowakabili.

## Mwana FA ajinadi kwa maji

Na Steven William, MUHEZA

SHILINGI bilioni 40 zimetolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka chanzo cha Mto Pangani kupeleka maji katika mji wa Muheza na vijijini ili kumtua ndoo mama kichwani ikiwa ni ilani ya Chama Cha Mapinduzi CCM.

Hayo yalisemwa na mgombea ubunge Jimbo la Muheza mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma (Mwana FA), wakati akizungumza na wananchi wa kata za Majengo, Genge, Makole na Potwe katika mikutano ya kampeni.

Alisema serikali imetenga fedha kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo cha Mto Pangani kupeleka Muheza mjini.

Mwana FA alisema kuwa miradi kama hiyo itatekelezwa katika miji 28 nchi nzima baada ya serikali ya Tanzania kukopa fedha Dola milioni 500 kutoka serikali ya India ambapo wakati wowote miradi hiyo itaanza kutekelezwa na makandarasi kutoka India.

## SAU:Tutashangaza wengi, tunaanza kesho, kisayansi

Ukurasa 13




# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 30, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

## Amy Coney Barret; Jaji kijana anayetingisha urais Marekani

# Kampeni vs w-ulemavu

## Ilikuwa wapi ilani nukta nundu, mafuta na kofia za alibino?

**Na Gaudensia Mngumi**

KUELEKEA uchaguzi mkuu Oktoba 28, walemavu wanapewa haki ya kutoa maoni na kusikika kupitia kampeni zinazoendelea? Nipashe, inasaka majibu kwa Mratibu Ukuzaji Mitaala na Upimaji Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Eligius Bwalya, anayeishi na ulemavu wa viungo na upofu, hapa anatoa ya moyoni...

**SWALI:** Unazungumziaje hali ya ulemavu na haki ya kujieleza na kusikilizwa wakati huu wa kampeni za uchaguzi mkuu kuwapata viongozi wa kuliongoza taifa, majimbo na kata?

**JIBU:** Kwa mujibu wa katiba ya Tanzania ya 1977 Mtanzania ana haki ya kusikilizwa na kujieleza (freedom of expression). Licha ya kuwapo kwa haki hii, utekelezaji wake kwa walemavu umekuwa midomoni mwa wanasiasa na viongozi wenye dhamana ya kuhakikisha haki hii inatekelezwa kwa vitendo.

Katika jamii yetu wenye ulemavu hawapati fursa ya kusikilizwa na kutoa maoni kupitia kampeni za udiwani, ubunge na urais zinazoendelea sasa kuelekea uchaguzi mkuu mwezi ujao. Ikumbukwe kuwa kuna makundi kadhaa ya walemavu ambayo yanasababisha kutofautiana kwa hali ya ulemavu na mahitaji yao maalumu baina ya mlemavu mmoja na mwingine. Hali hii hupelekea hata mahitaji yao kutofautiana, kwa mfano wapo wasioona, albino, viziwi, walemavu wa akili, viziwi-wasioona, walemavu wa viungo na wale wenye ulemavu mchanganyiko. Makundi yote haya yana mahitaji yanayotofautiana licha ya kuwa wote ni walemavu.

Nianze na wasioona, ni kundi ambalo lingependa kusikilizwa na kupewa fursa ya kutoa maoni wakati huu wa kampeni kwa sababu kuna ahadi na sera zinazotolewa kwa wananchi wakiwamo wasioona, lakini je, kuna mazingira na miundombinu wezeshi ili kupata haki hii ya kusikilizwa na kutoa maoni? Mazingira ya mikutano ya kampeni zinazoendelea yanafikika kirahisi na kundi hili? Wapo watu wa kuwaongoza wasioona (guiders) kufika maeneo ya kampeni bila tashwishi? Wasaidizi hawa wanapewa motisha gani ili waendelee na moyo huo huo wa kujitolea kuwasaidia wasioona kutembea kutoka eneo moja kwenda jingine?

**SWALI:** Ukichunguza ilani za uchaguzi zinawagusaje wasiiona?

JIBU: Pamoja na maswali yote haya, tafadhali pitia ilani za vyama vyote vinavyoendesha kampeni, je, kuna nakala ya ilani hata moja iliyoandikwa kwa maandishi ya nukta nundu ya wasioona? Yote haya yanahitaji kusikika katika vinywa vya wanasiasa na watawala kwenye kampeni zao na mwisho wa siku kuwajengea wasioona mazingira rafiki ya kusikilizwa na kuweza kutoa maoni yao juu ya mahitaji yao ya msingi.

**SWALI:** Kwa upande wa albino wakipaza sauti ili wasikike wakati wa kampeni watasemaje?

JIBU: Albino, katika kulinda mwonekano na unadhifu wa ngozi na utendaji mzuri wa macho yao, kundi hili linahitaji sehemu yenye kivuli, maandishi yaliyokuzwa, nguo nzito, miwani ya kulinda macho na mafuta maalumu. Wakati huu wa kampeni tungetamani kuona kundi hili linapewa fursa ya kusikilizwa na kueleza masuala yao



Bwalya anahoji mpigakura kama yeye anahitaji mengi. Fimbo, miwani, msaidizi, kitimwendo anawezaje kunufaika na haki za kikatiba kama uchaguzi, kutoa maoni na kusikilizwa? **PICHA: MWANDISHI WETU.**

na wanasiasa waeleze kwa namna gani na kwa kiasi gani wanazifahamu changamoto hizi na watazitatuaje mara tu wanaposhika hatamu ya kuongoza nchi.

**SWALI:** Vipi kuhusu walemavu wa viungo?

**JIBU:** Hawa wanahitaji miguu bandia, magongo, viti mwendo na baiskeli maalumu. Pia kama ilivyo kwa wasioona, walemavu wa viungo wanahitaji wasaidizi kwa ajili ya kuwahudumia kulingana na kukithiri kwa ulemavu na uhalisia wa vifaa aunyenzo kama vitimwendo (wheelchairs) na baiskeli zao kutokuwa na uwezo wa kujiendesha vyenyewe na hivyo kuhitaji mtu wa kusukuma.

Msaidizi ni lazima awe na moyo wa kujitolea kwani inabidi Maisha yake na muda mwingi autumie katika kumhudumia mwenye uhitaji. Kwa hiyo tungetamani kusikia kampeni zinazoendela zinasema nini kupitia ilani zao juu ya kuzikabili changamoto kama hizi.

"Hii inasababisha washindwe kupata fursa ya kujieleza na kusikika wakati huu kwani wengine hawana nyenzo za kuwapeleka mahali pa kampeni na pia kukosekana kwa wasaidizi wa kusukuma nyenzo hizo. Wachache wanaoonyesha moyo wa kujitolea hawana motisha.

**SWALI:** Viziwi-bubu wangependa kuona nini?

**JIBU:** Kundi hili pia lingependa kuona kampeni zinazoendela zinatoa fursa ya kusikilizwa na kutoa maoni. Suala hili limekuwa ni changamoto sugu kwa wanasiasa na watawala wetu kwani pale wanaposimama kunadi sera na ahadi kwa wananchi, husikii hata mwanasiasa anajipa muda wa kutaka kujua iwapo katika mkutano wake kama kuna watu wenye uhitaji maalumu kama hawa. Kutokana na hali hii, wanasiasa wala hawahangaiki na hata hawajishughulishi kutaka kujua mahitaji muhimu na maalumu ya kundi hili.

Kwa mfano, matumizi ya Lugha za alama na uwapo wa wakalimani kwenye matukio ya kampeni zinazoendelea ingewapa moyo walemavu wa uziwi/bubu kufuatilia kinachoendelea na hivyo kupata fursa ya kusikika na kueleza changamoto zao.

Viziwi-wasioona na wengineo wenye ulemavu mchanganyiko, hili ni kundi ambalo lina ulemavu ambao ama ni mzito au uliyokithiri kwa kuwa mtu anakuwa na upungufu au ulemavu zaidi ya mmoja. Mahitaji ya kundi hili ni mara mbili au zaidi ya makundi mengine. Hata mimi naangukia katika kundi hili kwani sioni na nina ulemavu wa viungo japo katika kuyakabili mazingira angalau kwa zaidi ya asilimia 50 ninamudu. Hii ni kutokana na mimi kupata fursa ya kwenda shule kwa kiwango cha shahada ya uzamili na pia ni mtumishi wa serikali kama Mratibu Ukuzaji Mitaala na Upimaji Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

"Hali hii ndiyo imesaidia angalau niweze kuyamudu mazingira ila bado haiondoi ukweli kuwa bado tunatamani kusikia wanasiasa na watawala kupitia majukwaa na mikutano yao wanasema ni kwa namna gani wanayafahamu mahitaji ya walemavu na hivyo kutoa fursa ya watu hawa kusikilizwa na kueleza changamoto zao"

**SWALI:** Unawashauri nini wa-

INAENDELEA UK.13

UCHAMBUZI

# Taifa linahitaji wenye maono kufikia maendeleo endelevu

**Na Dk. Felician Kilahama**



Cecilia Mwanga



Dk. Hussein Mwinyi



Dk. John Magufuli



Muttamwega Mgaywa



Queen Sendiga




Tundu Lissu

ILI Tanzania isonge mbele ipasavyo, inahitaji viongozi wenye uwezo na nia thabiti ya kuwaletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizoko kwa faida ya wote.

Siyo hivyo tu, bali pia viongozi wazuri wawe ni wenye uchungu na taifa hili. Hapa namaanisha wanaopenda amani idumu; siyo tu kwa kipindi cha uchaguzi hata baada ya hapo maisha yaendelee vizuri na wananchi waendelee kuwa na utulivu na hatimaye kupata maendeleo.

Maendeleo hayo yawe yenye uhakika na siyo maneno zaidi , vilevile, wawe wanaelewa umuhimu na faida za kushirikiana na kudumisha umoja na mshikamano.

Walinde Muungano wa Tanzania na Zanzibar hivyo tahadhali zichukuliwe za kuulinda kwa faida zetu ili amani na mshikamano udumu.

Nikiangalia utitiri wa vyama vinavyotaka kuingia ikulu najiuliza kulikoni? Je, ni suala la kugombania madaraka au kuna vivutio (vilivyofichwa nafsini mwa wagombea) kiasi kwamba lazima wagombee?

Sasa ni mapambano yenye changamoto nyingi ikiwamo maneno ya kukejeli, kulaumiana na kubeza hata mafanikio yaliyopo? Je, hali kama hiyo inaashiria nini kwa wapigakura?

Pengine wingi wa vyama nchini ni haki ya wanasiasa, ishara ya kinachoitwa demokrasia. Lakini iwapo katika nchi zilizoendelea tunakodhani demokrasia imeota mizizi kuliko mataifa yanayoendelea, unakuta harakati za kuongoza nchi zinahusisha vyama vichache, viwili au vitatu wakati kwetu ni vingi kulikoni?

Ninapojaribu kudadisi suala hili baadhi ya wadau wanatoa maoni kuwa sisi bado tuko nyuma sana hivyo ni fursa kwa wanasiasa kujikwamua kiuchumi (kujitajirisha) kwa kutumia migongo ya wapigakuara kuliko kuwaletea maendeleo.

Nchi zilizoendelea fedha wanazo nyingi zaidi kutafuta kuheshimiwa hivyo kuhusisha vyama vichache. Inaonekana pia wengi hatuna maarifa: kutokuwa na uelewa pamoja na upeo wa kutosha kuchambua na kupambanua uhalisia na ukweli wa wagombea tunabaki kushabikia tusiyoyajua.

Kwa mtazamo huo, tusiangalie vyama bali uwezo wa mgombea na hoja zake, Mfano, kama nia yake ni serikali tatu tujiulize kinachotafutwa ni nini? Je, Watanzania hatuwezi kuendelea kwa sababu ya serikali mbili badala ya tatu? Au nia ni kuwabebesha mzigo zaidi Watanzania (gharama za uendeshaji na mengineyo) kwa faida binafsi watu wachache?

Mara kadhaa nimemsikia Rais John Magufuli akisema "maendeleo ya Watanzania na taifa letu hayana vyama". Ni suala la kulifanyiakazi kwa bidii na kwa dhamira halisi ya kuwaletea watu maendeleo katika ujumla wake.

Katika hoja nyingine baadhi ya wagombea wanadai watu hawajapata maendeleo, "nguvu zimeelekezwa kwa vitu na siyo watu". Kauli kama hiyo inashangaza maana anayedai hivyo, tena kwa lugha ya kukejeli, ukimuuliza je, watu wataendeleaje bila kuwepo miundombinu imara? Hatakuwa na jibu la kuridhisha atabaki wa kulaumu tu. Juhudi zinazofanywa na serikali ni muhimu kwa maendeleo yanayolenga kuinua hali ya maisha kwa Watanzania wengi siyo wachache. Ili wakulima, wafugaji na wavuvi wafaidike na jasho lao, lazima kuwapo na uhakika wa chakula cha kutosheleza mahitaji ya familia lakini pia kuzalisha zaidi ili kuuza na kupata fedha. Inawezekana mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yakawapo ya kutosha lakini kama huduma nyingine hakuna itakuwa bado ni mahangaiko kuweza kupata fedha licha ya kuwapo chakula toshelezi.

Kazi kubwa ya serikali ni kujenga na kuimarisha huduma za jamii na miundombinu ili wananchi waweze kunufaika na kodi wanayolipa. Kimsingi, tunalipa kodi ili serikali itupatie huduma za msingi tuweze kujiendeleza na kunufaika kiuchumi. Serikali inajitahidi kufanya hivyo ili watu wote wanufaike na matunda ya kodi wanazolipa. Mkulima, mfugaji, mvuvi na wengineo walioko maeneo ya vijijini; wataweza kupata manufaa ya shughuli zao za kila siku iwapo huduma za kijamii zitaboreshwa katika ujumla wake.

Watalima, watafuga na watavua au kufuga samaki, iwapo wanapata huduma za afya karibu na kwa uhakika ili afya zao ziendelee kuimarika. Vilevile, afya itaboreka iwapo huduma ya uhakika ya maji ipo.

Wazazi watakuwa na amani mioyoni na kufanyakazi vizuri iwapo huduma za elimu ni bora. Huduma za ugani na elimu kwa umma zitakuwapo na kuimarishwa.

Hayo na mengineyo yanaunganishwa na miundombinu imara katika ujumla wake ikiwa ni pamoja na barabara, reli, usafiri na usafirishaji majini na angani.

Vilevile, tunazingatia miundombinu ya umeme, umwagiliaji, afya, elimu na usambazaji maji mijini na vijijini.

Kuweza kuyamudu hayo yote hatuhitaji siasa za maneno bali kwa vitendo vinavyotokana na dhamira ya kweli iliyomo ndani ya nafsi na maono na akili ya mtu na akawa na msimamo thabiti pamoja na nguvu za kuthubutu na kufanya kweli. Kwa hali ya kawaida (hata kiroho) tunakatazwa kusema uongo lakini katika siasa (hali isiyo kawaida) uongo eti unaruhusiwa.

Wadanganye wapigakura kwa kutumia ulimi-danganyifu kufanikisha malengo ya kisiasa na binafsi. Kwa mwanasiasa kusema uongo haoni shida wala kujutia kama anatenda dhambi kwa Mungu. Mathalani, ukisema mkinichagua fedha zitajaa mifukoni huku ukijua kuwa vigumu kuwafikia watu vijijini na wakati huo hujali uwepo wa miundombinu imara ni kuwahadaa wananchi. Watashangilia wakidhani itakuwa kweli kumbe ni uongo kisiasa.

Kimsingi ni kujituma na kufanya kazi kwa bidii "tutasema hali ni ngumu" lakini haitakuwa rahisi kwa maneno na kulalamika bali ni suala la kujitahidi kutumia nguvukazi zetu kibusara na kiutendaji.

Vilevile, tukumbuke hali ilivyokuwa Oktoba, 2015 na kabla ya hapo na sasa tuko wapi? Ukweli tumepiga hatua ya kutia moyo. Awamu ya tano imeingia madarakani na kuanza kushughulikia takribani sekta zote hata hivyo Mungu mwema, yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika ni kama miujiza fulani hivyo tunaelekea kujitegemea. Wanaolaumu na kubeza eti hakuna kitu hiyo ni hulka ya mtu mwenyewe.

Ni wajibu wa wapigakura kupima na kuchambua dhamira yake nini maana mwenye hulka ya kulaumu hata ufanye vizuri namna gani atalaumu tu.

Yeye anachotaka ni "nichague niingie madarakani mtaona matokeo". Ukisema iweje tusubiri kuona matokeo wakati tumeishayaona sasa tunataka kuongeza kasi ya kusonga mbele hatutaelewana maana mtazamo na malengo ni tofauti.

Kumbuka imenenwa "watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa". Wapigakura tuwe makini tusidanganyike kirahisi kwa faida binafsi bali tusonge mbele bila kupoteza muda.

Serikali ya sasa imethubutu, mengi yamefanyika yanatia moyo na "taa imeanza kutoa mwanga" tusiruhusu hoja za kutaka kuizima bila sababu za msingi.

# SAU: Tunaanza kazi kesho, tutawashangaza kisayansi



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha SAU, Muttamwega Mgaywa (kushoto), alipokuwa kwenye kampeni zake za awamu ya kwanza, eneo Kivukoni jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

**Na Sabato Kasika**

MGOMBEA urais wa Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa, baada ya kupumzika kwa siku kadhaa, anaibuka na kusema kutangulia si kufika, akijinadi kuwa atafanya kampeni za kisayansi na kwamba safari hii 'atapindua meza'.

Anasema ataanza ngwe mpya ya kampeni za kisayansi ambazo zitawashangaza wengi, hasa wasioamini kuwa SUA na wagombea wake wanaweza kufanya maajabu.

"Nimeacha wagombea wengine watangulie halafu ninakuja nyuma ili kubadilisha upepo wa kisiasa kwenye majimbo na mikoa ambayo tayari vyama vingine vimeshafanya kampeni zao," anatamba Mgaywa.

Anasema, ataitumia Oktoba kuzunguka nchi nzima kuomba kura kwa Watanzania wanyonge wakiwamo wakulima, aliosema SAU imepania kuwatetea kwa kuwa ndiyo wengi nchini.

Mgombea urais anasema, atasunda serikali ya kilimo na viwanda, kwa vile sekta hiyo ndiyo mkombozi wa Watanzania wote, hivyo anaahidi kuwa ni lazima kuwafikia wote. "Nikariri mithali isemayo 'kutangulia siyo kufika', hivyo wagombea wanaoendelea na kampeni si kwamba ndiyo wameshapata ushindi, nitakwenda kubadili upepo wa kisiasa," anaahidi.

Mgaywa anasema, jambo ambalo atazingatia ni kufanya kampeni za kistarabu bila kwenda kinyume na kanuni, taratibu na maadili ya uchaguzi, kwa maelezo kuwa wananchi wanataka sera si vinginevyo.

"Niwaambie wanachama, wapenzi wa chama chetu na Watanzania kuwa tupo imara na tunazunguka kufanya kampeni, kwani kimya kingi kina mshindo mkuu, tunawafuata huko waliko," anasema. Mwezi huu kuanzia Septemba 13, SAU ilizindua rasmi kampeni za mgombea urais, jijini Dar es Salaam, ambazo ziliambatana na uzinduzi wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Kampeni hizo zilifanyika kwa wiki moja, katika majimbo ya Ukonga, Ilala, Segerea na Kinondoni huku mgombea urais, akijinadi na pia kuwaombea kura wagombea ubunge wa majimbo hayo.

SAU ilisimamisha kampeni zake, huku viongozi wakisema lengo ni kufanya tathmini na kujipanga upya kwa ajili ya kuibuka katika awamu ya pili ya kampeni hizo.

Chama kimepumzika kwa zaidi ya wiki moja na sasa viongozi wanasema wako tayari kuendelea na kampeni mfululizo hadi Oktoba 27 ambayo ni siku moja kabla ya uchaguzi mkuu.

Katibu Mwenezi wa SAU Taifa, Awadhi Mtani, katika mahojiano na Nipashe, anasema, wataanza kampeni rasmi kesho."Zitakuwa za mfululizo, tutamalizia majimbo yaliyobakia Dar es Salaam ya Ubungo, Kibamba na Mbagala, kisha tutakwenda mikoani," anasema Mtani.

Anawataja baadhi ya wagombea wa majimbo ya Dar es Salaam kuwa ni Kunje Ngombale Mwiru wa Kibamba, Mwakasaka Donald wa Ubungo, Halima Mshana Kinondoni na Denis Tingo wa Mbagala.

"Wengine ni Joseph Kyara wa Ukonga, Bertha Mpata wa Segerea, Maria Kakili yuko Kawe wakati Amina Ahungu ni mgombea wa Ilala," anasema.

Anaahidi kuja na nguvu mpya, na kwamba muda ambao walipumzika, walifanya tathmini ya kutosha ambayo itawawezesha kufanya kampeni za kuwapa ushindi.

VYAMA VINGINE JE?

Wakati SAU inajiandaa kuanza awamu ya pili ya kampeni zake, baadhi ya vyama vimekwama kujinadi kwa wapigakura, kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya ukata

Baadhi ya wagombea hasa vyama vidogo, karibuni wanakaririwa na gazeti hili kwa nyakati tofauti, huku wakisema ukata umesababisha kufikia mikoa michache kwenye kampeni za kuwania urais.

Kwa mfano mgombea urais wa UPDP Twalib Ibrahimu Kadege, anasema hadi sasa ameifikia mikoa minne tu katika kampeni zake.

Kutokana na hali hiyo, anaweka wazi kuwa uwezekano wa kuifikia yote utategemeana na uwezeshaji na kwamba chama chao hakina ruzuku, badala yake wanachama ndiyo wanaochangishana fedha ili mgombea urais, aweze kusafiri mikoani kufanya kampeni.

Naye mgombea urais kupitia Demokrasia Makini, Cecilia Mwanga, anasema hadi juzi amefanya kampeni katika mikoa miwili tu na amepanga kufika mikoa minane tu.

Kwa upande wake mgombea wa urais wa Democratic Party (DP), Philipo Fumbo, anasema ameifikia mikoa minane hadi sasa, lakini anadhamiria kuifikia yote.

kwa upande wa chama cha NRA, mgombea urais Leopold Mahona, anasema tangu aanze kampeni amefanikiwa kuifikia mikoa 13, na anatarajia kuwafikia wagombea wa mikoa yote kwa kutumia helikopta kwa kufanya mikutano 20, kila siku.

Queen Sendiga, wa ADC, kwa upande wake anasema, hadi sasa amefanikiwa kuifikia mikoa minane tangu kampeni zimeanza.

Anafafanua kuwa mikoa mitano ni ya Zanzibar na mitatu ya Tanzania Bara, na kwamba atahakikisha muda uliobaki anaifikia mikoa yote na maeneo mengine anatumia mfumo wa kuwafuata wananchi katika maeneo yao, badala ya kuitisha mkutano wa hadhara wa kampeni.

Chama cha AAFP, mgombea wake wa urais Seif Maalim Seif, anasema ametembelea mikoa 15 katika kampeni na amepanga kuifikia yote na kwamba kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko ya jinsi ya kuendesha kampeni kwa kuachana kutumia mikutano ya hadhara ya kampeni, ambayo anadai ndiyo inakuwa kichocheo kwa baadhi ya wagombea kutoa kauli zinazohatarisha amani ya nchi.

# Kampeni vs wenye ulemavu

**INAENDELEA UK.13**

nasiasa kukumbuka haki hii kwa walemavu?

JIBU: Nisema haya, haki hii "ya kusikilizwa na kujieleza" inafinywa na wanasiasa hasa wakati huu wa kampeni, lakini kukosekana kwa utashi wa masuala ya walemavu, pamoja na wanasiasa na viongozi wengi kuongelea walemavu majukwaani, ukweli ni kwamba changamoto zao hawazijui kinagaubaga. Kwa hiyo wamekuwa wakiyaongelea masuala ya walemavu kwa ujumla bila kujali tofauti za ulemavu na mahitaji maalumu baina ya mlemavu mmoja na mwingine;

"Kukosekana kwa dhamira ya dhati ya kutekeleza mahitaji ya walemavu, kunaweza kutokea mazingira ambayo kwa kiasi baadhi ya wanasiasa na watawala wakazifahamu changamoto ambazo ni vikwazo kwa mustakabali wa maendeleo ya walemavu lakini bado ikakosekana nia au dhamira ya dhati ya kukabili changamoto hizo."

"Uwekezaji wa masuala ya walemavu na hasa mahitaji yao ni gharama kubwa lakini unahitajika uwekezaji wa kutosha kwenye masuala ya watu wenye ulemavu na wakati huu wa kampeni tulitamani kusikia wanasiasa wanasema nini juu ya hili"

**KUJISAHAU**

Wanasiasa na viongozi wengi wamesahau kuwa kama walivyo marehemu watarajiwa, vivyo hivyo wakumbuke pia ni walemavu watarajiwa kwani wanasafiri kwenye vyombo vya moto lakini wanaweza kukumbwa na matatizo ambayo hatima yake ni kupata ulemavu wa kudumu, ndiyo maana kuna usemi kuwa "kabla hujfa hujaumbika" ukimaanisha kuwa huna uhakika wa kuzikwa na viungo vyako kamili. Tunapopaza sauti kupigania haki au mazingira bora kwa walemavu, wakumbuke tunampigania kila mmoja . Kuwachukulia walemavu na changamoto zao kama tatizo ni kujitoa ufahamu na kusahau kuwa ulemavu unamhusu kila mtu wakati ukimfikia. Kwa hiyo wanasiasa na viongozi jengeni mazingira ya kuwawezesha walemavu kuyamudu mazingira kwa kuwatimizia mahitaji yao, kama nyenzo, vifaa saidizi, miundombinu na wataalamu yaani viti-mwendo, baiskeli maalumu, lugha ya alama, wakalimani, mavazi , miwani na mafuta maalumu.

# AMY CONEY BARRET; JAJI KIJANA ANAYETINGISHA URAIS MAREKANI

## •Wapinzani wa Trump wakwama kumzuia kupendekezwa, kuthibitishwa

**Na Ani Jozeni**

JAJI wa Mahakama za Rufani nchini Marekani, Amy Coney Barret, amekuwa sababu ya kiwewe miongoni mwa wafuasi wa chama cha Democratic na mgombea wa urais, Joseph Biden, wakipinga kutajwa kuwa jaji kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu wa nchi hiyo Novemba 3, mwaka huu.

Amy mwenye miaka 48, profesa wa sheria Chuo Kikuu cha Notre Dame jimboni Indiana nchini humo anapingwa na Biden na wenzake, wakisema kutajwa kuwa mbadala wa Jaji wa Mahakama ya Juu nchini humo Jaji Ruth Bader Ginsburg aliyefariki hivi karibuni akiwa na miaka 87.

Mahakama hiyo hutawaliwa na itikadi za uhafidhina dhidi ya uliberali, ndiyo maana zimewazonga wapiga kura nchini humo kwa wiki nzima na hatua hiyo inaonekana kuwa ni karata muhimu ya kura.

Sababu ya kutaka kumzuia Rais Donal Trump asimtaje mbadala wa hayati Jaji Ginsburg ni kuwa majaji wa mahakama hiyo ya juu zaidi nchini wanakalia viti vyao maisha yao yote, na kimsingi wanapiga kura kuamua kwa hisia zao jambo lolote linaloletwa mbele ya mahakama hiyo. Wachambuzi wa habari nchini humo wanasema kuwa atakapothibitishwa kuingia Mahakama ya Juu Jaji Barret ataongeza wingi wa majaji wahafidhina kutoka watano kwa wanne upande wa wafuasi wa uliberali, hadi kuwa sita kwa tatu. Na kwa vile majaji wa Mahakama ya Juu hawastaafu utakuwa unatetea masuala yanayopingwa na uliberali.

Wajumbe wa Baraza la Senate ambao wana dhamana ya kupitisha uteuzi wowote wa Ikulu ya Marekani kwa nafasi za juu serikalini au mamlaka kuu nyinginezo wanatazamiwa kumthibitisha kwa haraka iwezekanavyo.

Kiongozi wa kundi la maseneta wengi zaidi ambao ni Republican, Mitch McConnell, anahakikisha tangu wakati wa maombolezo ya Jaji Ginsburg kuwa Senate itampitisha mteule wa Rais Trump mara moja, kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu takriban mwezi mmoja ujao. Mgombea wa Democratic alitoa rai yenye hisia kali kwa maseneta wa Republican kuwa waadilifu kwa suala hilo na kutomthibitisha mteule yeyote hadi baada ya uchaguzi mkuu ujao.

Hata hivyo, wachambuzi wa siasa wanashangaa Democratic wanapiga kelele kuhusu uteuzi huo kwani wangekuwa madarakani wangefanya hivyo hivyo, kama ilivyotokea vipindi vingine vya urais nafasi ilitokea Mahakama ya Juu mmoja wa majaji anapofariki dunia. Kusema kuwa siyo uadilifu kutumia mwezi mmoja uliobaki kabla ya uchaguzi kufanya uteuzi na pia uthibitisho ndani ya kipindi hicho kunaleta hisia kuwa kujazwa nafasi hiyo na wahafidhina siyo 'uadilifu.' Uhafidhina nchini humo hasa ni kupinga utoaji mimba kiholela na ndoa za jinsia moja.

Hofu kubwa ya wapinzani wa Trump ni dhamira ya utawala wa Republican hivi sasa kubatilisha 'Affordable Care Act,' sheria ya mwaka 2010 ambayo ni urithi muhimu kutoka utawala wa Barack Obama wa kuwa na mfumo wa bima ya afya kuwafikia wote.

Kuna mijadala inayoendelea kuhusu uwezekano wa hatua hiyo kufanikiwa kwani katika awamu yake ya kwanza Rais Trump hakuwa na uwezo wa kufikisha kura zinazohitajiwa katika mahakama hiyo,



sa

kwani hadi zipatikane kura tano kwa nne, hukumu ipite. Ina maana jaji mmoja mhafidhina akipingana na mwelekeo huo ndiyo basi tena, ila mizania inapokuwa majaji 6-3 upande wa Trump, sheria hiyo iko mashakani.

Ikitoa taswira ya mwanamama huyo bingwa wa sheria, shirika la utangazaji la Uingereza BBC anasema kuwa ana watoto saba, na taarifa nyingine zinaelezea chuo kikuu alikoajiriwa, Notre Dame kama taasisi yenye maadili ya ndani ya Kanisa Katoliki na kwamba jina lake ni la Kikatoliki nchini Ufaran-

am-
ba-

lo mwaka juzi lilijikuta katika hitilafu ya umeme.

Moto ukaunguza na kuteketeza urithi wa sanaa za kuchora za karne zilizopita. Wachambuzi wanasema wapiga kura wa Trump wamefurahishwa mno na uteuzi huo, kwani ina maana kuwa inaweza ipite miaka 10 au zaidi kiitikadi kubakia hivyo mahakamani hapo.

Wako wanaosema kuwa endapo Trump atashindwa katika uchaguzi mkuu Baraza la Wawakilishi linaweza kutoa pendekezo, likubaliwe na rais mpya, kupanua idadi ya majaji katika Mahakama ya Juu ili ajenda za uliberali zisizuiwe kwa muongo mmoja au zaidi.

Rai hiyo inaashiria kuwa hakuna idadi ya juu ya majaji wa Mahakama ya Juu nchini humo iliyowekwa kikatiba, hivyo ikipanuliwa kuwa majaji 11 wakateuliwa wengine wawili waliberali mizania ingerudia mwanzo jambo ambalo wachambuzi wengi wanatingisha vichwa kama linaweza kufanikiwa.

Ili suala kama hilo lifanikishwe, ingebidi Democratic washinde kote - urais, na wingi mabaraza ya Senate nauUwakilishi, jambo ambalo si rahisi katika mazingira ya sasa. Ni kama tu limeshashindikana.

Kifo cha Jaji Ginsburg katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu na furaha ya wapinga uliberali nchini Marekani kupata mbadala wa mliberali Ginsburg aliye mwanamana na Mkatoliki mkereketwa ni ishara nyingine kuwa nyota ya Trump kuelekea uchaguzi mkuu inawaka vyema. Majuzi alifanikisha kuingia makubaliano ya kuondoa uhasama kati ya Israel na nchi mbili za Ghuba, Falme za Kiarabu na Bahrain ambao ni ushindi mkubwa wa kidiplomasia.

# Mch. ataka wananchi kujitokeza kupiga kura

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kwa wingi kwenye mikutano ya kampeni za uchaguzi mkuu 2020, kuwasikiliza wagombea ili kufanya maamuzi sahihi siku ya kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu.

Mchungaji wa kanisa la Talitha Cumi la jijini Dodoma, Daniel Kitua, alitoa rai hiyo jana jijini hapa wakati wa ibada ya kuliombea Taifa pamoja na Uchaguzi Mkuu.

Mchungaji huyo alisema ni wakati wa Watanzania kujitokeza kwa wingi kwenye mikutano ya kampeni zinazoendelea nchini ili kusikiliza sera za wagombea mbalimbali.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutambua sera za wagombea na kuzifanyia maamuzi sahihi ifikapo siku ya uchaguzi.

"Watanzania hivi sasa wanatakiwa kushiriki katika mikutano hii ya kampeni ili kupata fursa ya kusikiliza wagombea wanasera gani zitakazowasaidia kama watawachagua kuwa viongozi wao," alisema Kitua.

Kadhalika, aliwahimiza kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura ili kutimiza haki yao ya msingi ya kumchagua kiongozi wanayemtaka awaongoze kwa kwa kipindi cha miaka mitano.

"Na mkipiga kura Oktoba 28 mwaka huu mnatakiwa kurudi nyumba na kuziachia mamlaka husika kuendelea na zoezi jingine ikiwamo kutangaza matokeo na kutoziingilia katika maamuzi yake," alisema.

Aidha, alisema wanaombea Taifa ili Mungu amuinue kiongozi ambaye ataisaidia Tanzania katika maendeleo na kudumisha amani iliyopo.

"Tunaiombea pia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha kuwa Mungu anaiongoza katika kusimamia mchakato wote wa uchaguzi ili uwe huru na haki kwa kila upande," alisema.

Aliongeza: "Amani katika Taifa letu tumeilinda kwa zaidi ya miaka 60, sasa hatutapenda kuona mtu yeyote anakuja kuiharibu na kulifanya Taifa kuingia katika mifarakano yoyote."

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo, Naomi Chamene, aliwataka kinamama kuwa mfano kwa kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi huo kuanzia mikutano ya kampeni hadi upigaji kura.

**Amani katika Taifa letu tumeilinda kwa zaidi ya miaka 60, sasa hatutapenda kuona mtu yeyote anakuja kuiharibu na kulifanya Taifa kuingia katika mifarakano yoyote.**



Kijana akisaka wateja wa miche ya migomba katika Mtaa wa Mji Mpya, jijini Dodoma jana. Mche mmoja unauzwa kwa bei ya 5,000/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maaskofu, wachungaji kumtunuku JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS John Magufuli, kesho anatarajiwa kutunukiwa tuzo ya heshima na Chama cha Maaskofu na Wachungaji nchini (TPA), kutokana na kazi aliyoifanya kwa muhula wa kwanza wa uongozi wake.

Rais wa Chama hicho Askofu Musa Mlawi, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano la maombi ya kitaifa.

Mlawi, alisema kuwa tuzo hiyo itatolewa Oktoba mosi mwaka huu kwenye kongamano hilo lenye lengo pia la kuombea uchaguzi mkuu.

"Kongamano litafanyia katika viwanja vya Jamuhuri jijini Dodoma na Rais Magufuli, ndiye anayetarajiwa kuwa mgeni rasmi, hii tuzo tunaitoa kwa Rais kutokana na mambo makubwa aliyoyafanya katika kipindi cha uongozi wake wa miaka mitano," alisema.

Alibainisha mambo hayo kuwa ni pamoja na kuboresha miuondombinu na kuimarisha mahusiano kati ya serikali na viongozi wa dini nchini.

"Kongamano letu la maombi litajumuisha watu mbalimbali na kupitia maombi hayo yanakwenda kufungua baraka katika uchaguzi mkuu 2020, ili upite katika hali ya utulivu na amani kubwa," alisema.

Aidha, aliwataka Watanzania kuhakikisha kuwa wanajitokeza kupiga kura na kumchagua kiongozi bora atakayeongoza nchi kwa miaka mingine mitano.

"Wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani tumieni mikutano ya kampeni kunadi sera za vyama vyenu na kuacha kutumia lugha za matusi kuchafuana,"aliwaasa.

Kadhalika, aliitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kusimamia uchaguzi mkuu 2020, kwa kuzingatia miongozo na kanuni ili kila chama kipate haki kinayo stahili na kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza kila wakati katika chaguzi ulipita.

# DUWASA yapanua wigo upatikanaji wa maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA), imechimba visima vya maji vitano ili kuongeza upatikanaji wa maji jijini humo kutokana na kuwapo kwa ongezeko la watu baada ya serikali kuhamia Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi David Pallangyo, alisema visima hivyo vina uwezo wa kutoa maji lita 65,000 kwa saa kwa kisima kimoja.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji maji kutokana na mahitaji kuongezeka kutokana na ujio wa serikali.

"Tuliingia mkataba na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) ambao wapo chini ya Mamlaka ya Majisafi Vijijini (RUWASA) kwa ajili ya kuchimba visima 10 ili kuongeza upatikanaji wa maji," alisema.

Alibainisha kuwa mpango wa uchimbaji visima ni endelevu lengo ni kulifanya Jiji kuwa na maji ya kutosha.

Mhandisi Pallangyo alisema visima vitano vimeshachimbwa katika maeneo tofauti ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa maeneo mbalimbali.

"Dodoma itazidi kuwa na maji kwa sababu DUWASA tuna mikakati ya muda mrefu kuboresha mifumo ya maji," alisema.

Aidha, alisema wanatarajia kuanza kutoa maji Ihumwa kuleta Dodoma Mjini na hakutakuwa na kero ya maji. Alisema serikali ipo makini katika sekta ya maji ndio maana inaboresha mifumo ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliwatoa hofu wananchi kutokuwa na wasiwasi juu ya upatikanaji wa maji Jiji la Dodoma kwa kuwa DUWASA inaendelea kuimarisha upatikanaji wa maji maeneo yote ikiwamo ya pembezoni.

Kuhusu kuchimbwa bwawa la Farkwa, mkurugenzi huyo alisema kila kitu kipo tayari wanasubiri zabuni ili mchakato wake uendelee.

"Pia tuna mpango wa kuvuta maji Ziwa Victoria kuja maeneo ya mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma na tunaendelea na miradi ya uboreshaji maji katika maeneo tofauti zikiwa ni jitihada za kufikisha maji kwa kila Mtanzania," alisema.

**Pia tuna mpango wa kuvuta maji Ziwa Victoria kuja maeneo ya mikoa mbalimbali ikiwamo Dodoma na tunaendelea na miradi ya uboreshaji maji katika maeneo tofauti zikiwa ni jitihada za kufikisha maji kwa kila Mtanzania.**



# Mbeya-WSSA yaonya maji kutumika kisiasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEYA-WSSA), imewajia juu baadhi ya wagombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini wanaotumia miradi ya maji ya mamlaka hiyo, kupata umaarufu wa kisiasa kwa kuwaahidi wananchi kuwa wakishinda watawapelekea huduma hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Edna Mwaigomole, alisema moja kati ya miradi ambayo imekuwa ikitumiwa ni mradi wa maji wa Mto Kiwira ambao bado utekelezaji wake haujaanza na zinahitajika zaidi ya Sh. bilioni 75 kuutekeleza.

Alisema mamlaka hiyo ni ya daraja la 'A' na inajiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini na kwamba miradi mingi inatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani, hivyo akawataka wananchi kuwapuuza wanasiasa wanaojinadi kutumia miradi hiyo.

Mwaigomole alisema mamlaka hiyo ina vyanzo 16 vya maji vinavyohudumia Jiji la Mbeya pamoja na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na kwamba kati ya vyanzo hivyo 13 ni vya mito na vitatu ni vya visima.

**Lengo la Mbeya – WSSA, ni kuhakikisha mpaka kufikia mwaka 2025 upatikanaji wa maji katika Jiji la Mbeya na Mji Mdogo wa Mbalizi iwe asilimia 100.**

"Tunawaomba wananchi wawapuuze wagombea wanaodai wakichaguliwa watawaletea maji ya Mto Kiwira, huo mradi tulianza mchakato wake mwaka 2002 hatukuutekeleza kwa sababu hatukuwa na fedha za kutosha na tuliendelea na miradi mingine," alisema Mwaigomole.

"Kwa sasa tunaendelea na taratibu za kuanza kuutekeleza kwa sababu usanifu wa miradi iliyopo kwa sasa ilikuwa inatosheleza mahitaji ya wananchi na shughuli zingine mpaka mwaka 2017 na kwa sasa tuna mahitaji ya maji ni lita milioni 70 kwa siku, lakini uzalishaji ni lita milioni 40 hivyo tumeongeza nguvu ya kuutekeleza mradi huo," alisema.

Alisema lengo la Mbeya - WSSA, ni kuhakikisha mpaka kufikia mwaka 2025 upatikanaji wa maji katika Jiji la Mbeya na Mji Mdogo wa Mbalizi iwe asilimia 100.

Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alisema mamlaka hiyo imeanza harakati za kutekeleza mradi wa maji wa Mto Kiwira na kwamba makadirio ya gharama za mradi huo ya mwaka 2016 wakati upembuzi unafanyika ilikuwa Sh. bilioni 75.

Alisema ili kuukamilisha wanahitaji msaada wa serikali pamoja na wahisani kutokana na gharama hiyo kuwa kubwa ambayo mamlaka haiwezi kumudu na kuukamilisha kwa wakati.

Mhandisi Mengo alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ya Mamlaka hiyo, wametenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa baadhi ya shughuli ikiwamo kuwalipa fidia wananchi watakaoathiriwa na mradi na kuanza ujenzi wa chanzo.

"Ili mradi ukamilike kuna shughuli kuu tano ambazo tutahitaji kuzifanya ambazo ni kujenga chanzo, kujenga njia mpaka kwenye eneo la kutibia maji, kujenga eneo la kutibia, kulaza bomba mpaka hapa mjini na kujenga tangi kubwa la kuhifadhia," alisema Mengo.

Alisema kutoka kwenye chanzo cha maji hayo mpaka Mbeya Mjini kuna umbali wa kilomita 55 na hivyo kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuyafikisha maji mjini.

Alisema mbali na maji hayo kutakiwa kulinufaisha Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi pia kuna vijiji saba vya Wilaya za Rungwe na Halmashauri ya Mbeya ambavyo vinapitiwa na mradi huo vitanufaika ili kuimarisha ulinzi wa miundombinu.

Mei mwaka jana wakati wa ziara ya Rais John Magufuli mkoani Mbeya, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu', aliomba mradi wa maji wa Mto Kiwira ukamilishwe na kwamba utakuwa suluhisho la tatizo la huduma hiyo na pia kwenye kampeni zake amekuwa akidai kuwa atahakikisha unakamilika.



Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya, wakifanya usafi kwenye soko la wamachinga lililopo eneo la uwanja wa zamani wa ndege jijini humo, mwishoni mwa wiki ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la serikali la kufanya usafi kila mwisho wa mwezi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mgombea CHAUMA kugawa matrekta

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Protas Mgimbila, amesema endapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, atagawa matrekta kwenye mitaa yote ya kata za pembezoni mwa mji ili wananchi wayatumie kwenye kilimo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa anazindua kampeni zake katika Kata ya Uyole jijini humo, ambapo alisema lengo lake ni kuimarisha kilimo cha viazi mviringo, ngano na mahindi ili wananchi wajitosheleze kwa chakula na kipato kwa kuuza ziada. Mgimbila alizitaja kata anazozilenga ni Iziwa, Iduda, Mwansekwa, Mwakibete na Iganjo, na kwamba matrekta ambayo anakusudia kuyagawa ni ya kisasa na yatawasaidia wananchi hao.

"Wengi wa wakulima wetu wa kata hizo wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea ambacho hakiwezi kuwakomboa, sasa mimi nakuja kuwasaidia kuboresha sekta hiyo muhimu kwa ajili ya maisha yenu," alisema Mgimbila.

Alisema baadhi ya wagombea wa vyama vingine wamekuwa wakiwatenga wananchi wa kata hizo za pembezoni na kuishia kuwahudumia wa kata za mjini zaidi na kwamba yeye atahakikisha anaweka usawa.

Alisema atahakikisha barabara zinazoelekea kwenye maeneo ya mashamba zinaboreshwa ili kuwarahisishia wananchi wa maeneo hayo kusafirisha pembejeo kwenda mashambani pamoja na kusafirisha mazao kwenda sokoni.

Katika hatua nyingine Mgimbila alisema atahakikisha barabara zote za mitaa ndani ya Jiji hilo zinajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwarahisishia wananchi kusafiri na kupunguza msongamano wa magari katikati ya mji.

Alisema mbali na kujenga barabara za mitaa, pia atahakikisha anaweka taa zinazotumia mionzi ya jua kwenye mitaa mbalimbali ili kuwadhibiti vibaka ambao wamekuwa wakiwapora wananchi mali zao hasa nyakati za usiku.

# Waandishi washauriwa kujiimarisha kiuchumi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANDISHI wa habari mkoani Mbeya wameshauriwa kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha miradi itakayowaongezea kipato na kujiandalia maisha mazuri baada ya kustaafu kazi hiyo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa anazungumza na waandishi hao kuhusu shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo serikali imetekeleza ndani ya mkoa huo ukiwamo utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali.

Chalamila alisema kundi la waandishi ni miongoni mwa makundi ambayo yangenufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri, lakini tangu mikopo hiyo ilipoanzishwa hakuna kikundi hata kimoja cha wanatasnia hao kilichojitokeza kuomba.

Alisema waandishi wakijiimarisha kiuchumi watakuwa na nafasi ya kufanya kazi zao kwa uhuru na kwa ufanisi na kwamba hakuna wadau ambao watakuwa wanawadharau.

"Kuna umri mtafika hamtakuwa na nguvu za kukimbizana kama mnavyofanya sasa hivi, sasa ni vizuri mkaanza kuweka mapema ili mkifikia umri huo mpumzike mkiwa na maisha mazuri, msitegemee mishahara pekee," alisema Chalamila.

Alisema hata yeye wakati anaenda kujiunga chuo kikuu kwa mara ya kwanza alichaguliwa kwenda kusoma fani ya uandishi wa habari, lakini alibadili fani na kwenda kusoma ualimu.



# TAMWA yatoa mafunzo dhidi ya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Action Aid kimewapatia mafunzo ya kupambana na udhalilishaji wa kijinsia wananchi 660 kutoka Shehia 22, Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Mwanasheria kutoka TAMWA Zanzibar, Zaina Salum Abdala, alisema lengo kuu la kutoa mafunzo hayo kwa wananchi ni kuwajengea ufahamu dhana nzima ya udhalilishaji na madhara yake kwa sababu bila kuwa na elimu sahihi ya matendo hayo hayataweza kumalizika.

Alisema kuwa elimu hiyo iliyotolewa kwa muda wa wiki mbili kwa wananchi hao italeta mabadiliko makubwa ikiwamo kufahamu viashiria vya udhalilishaji na umuhimu wa kutoa taarifa matukio hayo yanapojitokeza kwenye jamii.

Alisema kuwa katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar hadi sasa baadhi ya wanajamii wamekuwa wakiyafumbia macho matendo hayo kutokana sababu mbalimbali ikiwamo kuhofia kuvunjika kwa ndoa zao.

**Kuna matukio mbalimbali ya udhalilishaji yanafanyika, lakini watu wapo tayari kuona yanaendelea na hushindwa kusema kwa kuhofia kupewa talaka na waume zao.**

"Kuna matukio mbalimbali ya udhalilishaji yanafanyika, lakini watu wapo tayari kuona yanaendelea na hushindwa kusema kwa kuhofia kupewa talaka na waume zao," alisema.

Hata hivyo, mwanasheria huyo aliitaka jamii kubadilika na kuondokana na usiri kwa kutoa taarifa dhidi ya matendo hayo kwa lengo la kuchukuliwa hatua kali zaidi kwa watendaji wote watakaobainika.

Akizungumza kwa niaba ya masheha wenzake, sheha wa shehia ya Kitope, Khamis Ndende Juma, alisema wanakabiliwa na matukio mbalimbali ya udhalilishaji kwenye jamii hali ambayo wengi wameanza kushtuka na kuhofia madhara zaidi.

Alisema usiri bado ni tatizo wanaloendelea kukabiliana nalo ndani ya jamii zao kwa kuwa wapo baadhi ya watu wanatendewa matendo hayo na kisha kuamua kunyamaza kimya.

Sheha huyo alisema kupitia elimu hiyo iliyotolewa na TAMWA italeta mafanikio na watu kuwa tayari kutoa ushirikiano wa kina dhidi ya matendo hayo kwa lengo la kuyamaliza kabisa.

Mwananchi Ali Makame kutoka shehia ya Kitope alisema ili jamii iweze kumaliza tatizo hilo wazazi na walezi wawe karibu zaidi na watoto wao muda wote. Alisema matukio mengi yanayotokea yanaonyesha kuwa baadhi ya wazazi ama walezi wamekosa umakini wa kuangalia watoto na wakati mwingine huwa sababu ya kufanyiwa unyama huo.

Kwa upade wake Ofisa Dawati la Jinsia, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Salum Khamis Machano, alisema licha ya jitihada zinazofanywa na dawati hilo kwa kushirikiana na wanaharakati mbalimbali, bado kuna tatizo ndani ya jamii ikiwamo la kukosa utayari wa kuendelea na baadhi ya kesi ambazo huwa zimeshafikishwa katika vituo vya polisi.

Aliomba jamii kubadilika na kuyachukuliwa matendo hayo kuwa ni ya kinyama na yasiyoopaswa kuvumiliwa kwa mtu yoyote.

# Ataka wazazi, walimu kudhibiti utoro shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi, Safia Ali Rijali, amewataka walimu wakuu, wazazi na kamati za shule kushirikiana kudhibiti tatizo la utoro, udhalilishaji, mimba na ndoa za umri mdogo ili watoto wanapata haki yao ya msingi ya elimu.

Alisema hayo huko Mkwajuni Wilaya ya Kaskazini 'A' wakati akizungumza na walimu na wazazi wa shule za maandalizi na msingi kuhusu maendeleo ya watoto ili kuepukana na vitendo viovu.

"Mimba za umri mdogo na ndoa za mapema na utoro shuleni ndio chanzo kikuu kinachorudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa watoto," alisema Safia.

Alisema ukosefu wa elimu kwa mtoto kunasababisha kukosekana kwa wataalamu nchini na ongezeko la vitendo viovu ikiwamo udhalilishaji.

Kwa upande wa mwasilishaji mada kuhusu utoro shuleni, Ofisa Elimu Maandalizi na Msingi, Ame Juma Khatibu, aliwataka walimu kuweka utaratibu wa kuwakagua wanafunzi pia kuunda kamati maalum kwa ajili ya doria ili kuudhibiti utoro kwa wanafunzi.

Alisema sababu za utoro ni kukosekana kwa ushirikiano kati ya wazazi, walimu na kamati katika kusimamia vizuri majukumu yao.

"Kuacha utoro uendelee ni njia moja wapo ya kuvunja haki ya mtoto," alisema Ame.

Aliwaomba walimu na wazazi wachukue hatua za kuanzisha utaratibu wa kuwasaidia wanafunzi wenye mazingira magumu ili watoto wote waweze kupata haki yao ya msingi ya elimu.

Ofisa Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi, Asya Hassan Mussa, alisema kuficha ukimya baada ya mabadiliko ya kimwili ya msichana na mvulana kunasababisha athari za mimba ndoa na udhalilishaji.

Pia, alieleza madhara ya mimba za utotoni na udhalilishaji ni pamoja na kukatisha masomo, kupatikana kwa maradhi mbalimbali pamoja na kujenga uhasama katika jamii.




Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa (wa pili kulia), akizindua nembo ya Benki ya NCBA Tanzania, katika hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la benki hiyo, mjini Zanzibar. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa NCBA, Margaret Karume, Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Hassan Hafidh (kushoto) na Mshauri wa Rais wa Zanzibar, Abdulrahman Mwinyimbegu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji aomba viongozi wa dini kuombea uchaguzi amani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud, amewataka viongozi wa dini kuendelea kuiombea nchi amani ili iendelee kuwa salama hasa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa uchaguzi wakiwamo na viongozi wa dini, alisema wakati kampeni zikiendelea hadi sasa hakuna tukio la uvunjifu wa amani lililoripotiwa na kampeni hizo zinaendelea vizuri kwa amani na ustaarabu.

"Tunakuombeni mwendelee kushiriki katika kuhamasisha kampeni na hatua nyingine za uchaguzi kwa utulivu na amani ili nchi yetu iendelee kuwa visiwa vya amani," alisema.

Pia, alisema Tume inatambua umuhimu wa viongozi wa dini kwa sababu wanaongoza kundi kubwa la jamii na kuwa na nguvu kubwa ya ushawishi kwa waumini wao.

Aliwataka wadau hao kuendelea kuhubiri amani kwa wananchi wote kabla na baada ya uchaguzi, pia kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii ili iweze kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

"Naomba ifahamike kuwa kutunza amani ni wajibu wa kila mwananchi katika taifa hili, kila mmoja wetu atumie muda wake kuitunza amani iliyopo na kwa upande wetu Tume ya Uchaguzi tunaendelea kuhamasisha wapigakura wote kupiga kura kwa amani," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Tume hiyo, Thabit Idarous Faina, alisema matayarisho ya uchaguzi mkuu yamekamilika ikiwamo ununuaji wa vifaa kwa ajili ya uchaguzi.

Alisema kuwa gharama zote za uchaguzi mkuu wa mwaka huu zimegharamiwa na Serikali ya Zanzibar na haijategemea fedha za wafadhili kama ilivyozoeleka katika chaguzi zilizopita.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**BEACH PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 0.91 Acres (3682.64 Square Meters)
LOCATION: - PLOT NO 40, KUNDUCHI BEACH, NEXT TO SILVER SANDS,DARESALAAM CITY
DESCRIPTION: - DIRECT ACCESS TO THE BEACH.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

## VIWANJA/MASHAMBA

**Eneo linapangishwa/kuuzwa**
Eneo linapangishwa/ kuuzwa ukubwa wa mita mraba (sqm) 3,130, Tabata Liwiti, Dar es Salaam. Liko katika barabara kuu na inafaaa kwa ajili ya kujenga kituo cha mafuta, super market nk. Wasiliana kwa simu: 0715624747/0767235965.

## VIWANJA/MASHAMBA

**PRIME PLOT FOR SALE**
PLOT SIZE: - 14.87 HECTARE (36.74 ACRE)
LOCATION: - BAGAMOYO DISTRICT, BLOCK C SANZALE, LOCATED ON MAIN ROAD, 5 MIN FROM BAGAMOYO TOWN,3 KM AWAY FROM ROUND ABOUT
DESCRIPTION: - THE PLOT IS FURTHER DIVIDED IN 5 DIFFERENT TITLES.
INTRESTED BUYERS MAY CONTACT +255 753786114

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**Herieth Ernest Msagati** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidatocha nne chenye **index namba P2517-0198** lilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari Alfagems . Yeyoteb atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MBA/RB/652087/2020**

115920702

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo NYALIKUNGU**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 19/2020**

**Ombi la SAMWEL LOTH MWANGA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu LOTH MASENGA MWANGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 05/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/09/2020.

HAKIMU MKAZI

115922302

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDICIARY)**

**KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO**

**SHAURI LA TALAKA NA. 27/2020**

**MDAI.....ABEL KISAKYE & WENZAKE 27**

**DHIDI YA**

**MDAIWA.......MARGERETH SARAMAKI STEPHEN & WENZAKE 2.**

**KWA: 1. MARGERETH SARAMAKI STEPHEN**
**2. BENROSE TANZANIA LIMITED**
**3. DEOGRATIAS R. KAMUGISHA**

**POPOTE ULIPO.**
Mahakama hii inawafahamisha kwamba waombaji wamefungua kesi ya madai dhidi yenu,nakala ya madai hayo inapatikana katika Mahakama hii.

Shauri limepangwa kusikilizwa Tena tarehe 19/10/2020 saa 2:30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo,au kuwakilishwa kisheria pamoja na kuleta utetezi wenu dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutokufika kwenu tarehe hiyo,shauri litaanza kusikilizwa Bila ya nyie kutaarifiwa tena,na maamuzi kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI MOROGORO

115922502

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA 63)**

**SHAURI LA MADAI NO 13/2020.**
**Mahakama ya mwanzo : Nyakaliro**
**Wilaya: Sengerema**

**Mdai: Silivester Lweganza KNY kikundi**

**Mdaiwa: 1 Jeniroza John 2. Aron Wilson**

**Kwa : 1 Jeniroza John 2. Aron Wilson**
**K.K. Mwenyekiti wa kitongoji Nyanuswi kusini.**

Kwa kuwa mdaiwa/ wadaiwa ameleta/ wameleta yake/ yao kwamba eleza habari ya madai kwa ajili ya kujibu dai la Tshs 891,200/= laki nane na elfu tisini na moja na mia mbili kwa hiyo unaitajika mnaitajika kuhudhuria kwa binafsi katika mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 01/10/2020. Asubuhi kwa kujibumadai haya na kwa kuwa siku hiyo tajwa shauri hilo/ kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo Angalia kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ Mmeshindwa. Tarehe 28.09.2020

**Hakimu mahakama ya mwanzo**
**HAKIMU MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**NYAKARILO**

115922202

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAHARANI ALLY MASIMBA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI T160 DRD
**CHASSES NO T30001490**
**ENGINE NO QR20021136A**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**ARU/ARU/RB/330425/2020.**

115922402

## KUPOTEA KWA PASPORT



**DICKSON ELIAFIE LEMA**
Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, **TAE 222513** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji October 2019 Dar Es Salaam.
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**KL/MOS/RB/700049/2020**

115921402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA MADAI MAOMBI NA. 3/2020**

**TECHNICS CONSTRUCTION GROUP LIMITED....... MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **AGAPE SANCTUARY MINISTRIES INTERNATIONAL TANZANIA LIMITED.........WAJIBU MAOMBI KWA:**
1. **AGAPE SANCTUARY MINISTRIES INTERNATIONL TZ LTD.**

**POPOTE WALIPO**

**YAH. TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA MADAI MAOMBI NA. 3/2020 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya MHE. JAJI G. M. MASAJU, wa Mahaka kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya jumanne tarehe 20/10/2020.
**HIVYO;** Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Wakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** Hamtafika nyinyi au wakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na mahakama kama itavyoamua pasipo nyinyi au wakili wenu kuwepo
IMETOLEWA; Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakam leo hii tarehe 22/09/202.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

115922002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Usimamizi wa Mirathi**

**Ombi la MARCO PAUL LWANZEGA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu TINA EXAUD KOKA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 28/09/2020.

115922102

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DARE ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 48 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**MOHAMED HAMIS ABDALLAH**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI ABDULLATIF MOHAMED HAMIS**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji /Mwaombaji hapo juu, Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe....Mwezi wa September....2020 .

Imewasilishwa Dar Es Salaam,leo tarehe 23 mwezi wa September 2020

NAIBU MSAJILI

115921302

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**MAOMBI NO. 134/2020**

**DOUGLAS AUGUSTINE MAGOMBOLA:::::::MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**SOPHIA ALPHONCE MWENDA**
**SHUKRANI MWAKIBINGA** } **:::::::WAJIBU MAOMBI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: SOPHIA ALPHONCE MWENDA**

Fahamu kwamba maombi yamefunguliwa dhidi yako katika baraza hili. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 20/10/2020 saa2: 30 asubuhi mbele ya Mh. A. Mapunda mwenyekiti wa baraza. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini
Kumbuka: Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewaa kwa mkono wangu na Lakiri/ Muhuri wa baraza hili umetolewa leo tarehe 24/09/2020

A. Mapunda
mwenyekiti

115921102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAHATI BONIPHACE KAZUZU**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA COASTER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 623 DSA**. CHASSIS NAMBA **HDB510005755.**
ENGINE NAMBA **1HD0182722.**
YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
**Control No: 9910819244002.**

115921502

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042,**
**Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Medali aliyotunukiwa panya yawaibua watafiti

**Na Beatrice Moses,** TUDARCO

MEDALI ya dhahabu aliyotunukiwa panya Magawa, akitajwa kujitolea kwake kuokoa maisha kupitia kazi yake ya kubaini mabomu hatari yaliyotegwa ardhini nchini Cambodia, imetajwa kuwa ni chachu kwa kituo chake cha kazi Tanzania.

Akizungumza na Nipashe, Mtafiti wa Kituo cha Utafiti na Udhibiti wa Viumbe Hai Waharibifu wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Dk. Georgies Mgode, alisema wamepokea kwa furaha taarifa za mafanikio ya panya huyo, ambayo yametambulika kwa kiwango cha kimataifa.

Alisema ni chachu kwa SUA katika kazi zao za utafiti wanazoendelea kuzifanya, kwa kuwa hayo siyo mafanikio ya panya pekee bali waliotafiti na waliotoa mafunzo kwa ujumla.

"Pia tunajivunia kwa kuwa serikali imechangia mafanikio haya kwa kuwa ilipiga marufuku kusafirisha wanyama hai nje ya nchi, lakini kwa kutambua umuhimu wa utafiti iliruhusu kusafirishwa kwa panya hao hatimaye matunda yanaonekana sasa," alisema.

Alisema wanaendelea kufanya utafiti wa panya wanaotambua makohozi yenye bakteria wanaosababisha kifua kikuu, ambapo kwa nchini wameonyesha umahiri wao kwa kugundua watu 1,500 lakini bado hawajathibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kwa taarifa kutoka kwenye mtandao wa Shirika la Utangazaji la BBC, Magawa amefanikiwa kunusa mabomu 39 na silaha 28, ambazo hazijalipuka katika maisha yake, inadhaniwa huenda kuna hadi mabomu milioni sita ya kutegwa ardhini Cambodia ya kusini mashariki mwa bara la Asia.

Imebainisha kuwa, Shirika la matibabu ya wanyama la Uingereza lisilokuwa la kiserikali PDSA, limemtuza medali ya dhahabu panya huyo, ambayo imeandikwa maneno "Kwa juhudi za wanyama au kujitolea kazini".

Panya huyo aliye na miaka saba, alipewa mafunzo na shirika lisilo la kiserikali- Apopo kutoka Ubelgiji lenye makao yake Tanzania, kwa wanyama 30 waliopewa tuzo hiyo, huyu ni panya wa kwanza. Shirika hilo limekuwa likiwalea wanyama wanaofahamika kama - PanyaShujaa- kugundua uwapo wa mabomu ya kutegwa ardhini tangu miaka ya 1990.

# Miradi barabara EAC yatekelezwa kwa kasi

**Na Enock Charles**

UTEKELEZAJI wa miradi ya miundombinu chini ya Mtandao wa Miradi ya Barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Road Network Project-EARNP), yenye dhamira ya kuunganisha nchi wanachama za jumuiya hiyo, unaendelea kushika kasi kwenye maeneo mbalimbali ya mipaka baina ya nchi hizo.

Lengo la utekelezaji wa miradi hiyo ni kuongeza kasi ya biashara miongoni mwa mataifa wanachama.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Wilbert Ibuge, alipotembelea mradi wa barabara kutoka Nyakanazi -Kasulu hadi Manyovu wenye urefu wa kilomita 310, ambao unahusisha pia ujenzi wa Kituo cha Huduma kwa Pamoja cha Manyovu/Mugina na Daraja la Mto Malagarasi.

Ujenzi huo, ambao kwa kipande cha Nyakanazi Kibondo/Kabingo chenye urefu wa kilomita 50 umeanza kutekelezwa kwa fedha za Serikali ya Tanzania.

Aidha, Serikali ya Tanzania imetoa zaidi ya Sh. bilioni 13, kwa ajili ya kuwafidia watakaopitiwa na barabara hiyo, ambapo waathirika zaidi ya asilimia 93, wameshalipwa fidia zao na asilimia saba iliyosalia watalipwa hivi karibuni, baada ya wao kufanya marekebisho ya kasoro zilizojitokeza.

Balozi Ibuge alieleza kufurahishwa na maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo, ambapo alitumia fursa hiyo kuwasihi makandarasi waendane na kasi na ari ya serikali ya kuhakikisha kuwa barabara hiyo inakamilishwa mapema kabla ya muda uliowekwa wa miaka mitatu.

Alisema, ujenzi wa miundombinu hiyo inasaidia kuongeza kasi ya mwingiliano wa watu baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo ni moja ya sera kuu ya nchi hizo.

Kadhalika, alisema sio tu ujenzi wa miundombinu hiyo utarahisisha biashara ya bidhaa na huduma baina ya nchi za jumuiya, bali pia utaongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa sababu ya uhakika wa soko katika nchi wanachama.

Balozi Ibuge alitumia fursa ya ziara hiyo, kutembelea kambi ya wakimbizi ya Nduta na kuzungumza na mkuu wa kambi hiyo, kuhusu masuala mbalimbali, ikiwamo kuwarejesha wakimbizi kwa hiari katika nchi zao.




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel (wa pili kulia), akikabidhi mfano wa funguo ya Excavator (tinga tinga) mchimbaji mdogo wa madini wa mkoa huo, Ezekiel Rembo, baada ya kununua kutoka kampuni ya Gf Truks & Equipments kwa punguzo la 20%, wakati wa maonyesho ya tatu ya sekta ya madini mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango wa mbolea bure waanza Kigoma

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amezindua mpango wa kugawa mbolea bure kwa wakulima wadogo unaoratibiwa, na kuwataka wakulima kutumia fursa hiyo kuongeza wingi wa mpunga na mahindi.

Akizungumza hapa kwenye uzinduzi wa mpango huo, unaojulikana kama 'ActionAfrica' na unaolenga kugawa tani 125,000 za mbolea zinazokadiriwa kuwa na thamani ya Sh. bilioni 16.5, Andengenya alisema kama mbolea hiyo kutoka Kampuni ya YARA Tanzania, itawafikia wakulima na wakaitumia vizuri, utakuwapo uhakiki wa kupata chakula na pato la wakulima kuongezeka.

"Ni mpango mzuri na unaopaswa kupongezwa na kila mpenda maendeleo ya wakulima wa nchi hii, kwani utaongeza upatikanaji wa chakula na pia kipato cha mkulima mmoja mmoja hapa nchini na cha Taifa kwa ujumla," alisema.

Aidha, aliwahimiza wakulima mkoani humo kujisajili, ili waweze kunufaika na mpango huo kwa kupiga simu *149*46*16#.

RC Andengenye ameziomba kampuni nyingine zinazosambaza zana na pembejeo za kilimo kuiga mfano wa YARA, ili kuzidi kuimarisha sekta ya kilimo, ambayo inaajiri Watanzania wanaokadiriwa kuwa ni asilimia 65.

Meneja wa Biashara wa YARA, Kanda ya Magharibi, Phillipo Mwakipesile, alipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuunga mkono jitihada za YARA hapa nchini.

"Shukurani zetu ziende kwa Wizara ya Kilimo kwa namna ambavyo imetuunga mkono kwa kipindi chote cha miaka 15 ya uhai wa Yara Tanzania. Tunaamini tutafanya makubwa zaidi siku za usoni kwa manufaa ya wakulima na maendeleo ya Tanzania kwa ujumla," alieleza Mwakipesile.

# SOLSKJAER: SIHITAJI BEKI KWA SASA




**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United kwa sasa haina uhitaji mkubwa wa kupata mlinzi, kwa sababu anaamini wachezaji alionao ni imara na wanaweza kumpa mafanikio.

Solskjaer yupo kwenye presha kubwa hasa baada ya kufungua pazia la Ligi Kuu England kwa kupokea kichapo cha mabao 3-1, mbele ya Crystal Palace kabla kushinda mabao 3-2 mbele ya Brighton, mwishoni mwa wiki.

United imemwongeza nyota mmoja kikosini kwake, ambaye ni kiungo Donny van de Beek, huku maswali mengi yakiwa ni kuhusu pacha ya mabeki kati ya Harry Maguire na Victor Lindelof.

Lakini, Solskjaer amesema kwamba kwa sasa haitaji beki kwani kikosi chache kinajitosheleza katika nafasi hiyo.

"Kwangu mimi ninaona kwamba tuna safu imara ya mabeki kwa muda huu kilichoshindikana ni muundo pekee, muundo ukiwa mzuri basi tutafanya vema. Makosa ya mtu binafsi ni madogo sana," amesema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

Hata hivyo, wachambuzi wengi wa soka wanaona kwamba, United ina tatizo kubwa la ulinzi na hivyo wanaweza kujiweka kwenye wakati mgumu, kwenye mbio za Ligi Kuu ya England msimu huu.

## Conte akomaa na Kante

**MILAN,** Italia

INTER Milan ipo kwenye mpango wa kuipata saini ya kiungo wa Chelsea raia wa Ufaransa, N'Golo Kante msimu huu licha ya kukutana na vigingi kutoka kwa mabosi wake.

Antonio Conte alishinda taji la Ligi Kuu England akiwa na Kante wakati alipokuwa ndani ya Chelsea, hivyo anakubali uwezo wake na anajua namna ya kumtumia iwapo atampata ndani ya Klabu ya Inter Milan.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka Italia, zimeeleza kuwa, ili Inter Milan waipate saini ya nyota huyo ni lazima wamuuze mchezaji wao mmoja, ili kufikia malengo ya dau la nyota huyo, ambalo linatajwa kuwa ni euro milioni 46.

Chelsea hawana mpango wa kumuuza nyota huyo, kwani walipokea ofa, ambayo iliwahusisha wachezaji wawili, ambao ni Christian Eriksen and Marcelo Brozovic.

Miamba hiyo ya Italia inahitaji saini ya Kante mwenye umri wa miaka 28, ili kuongeza nguvu ndani ya kikosi chao, ambacho kinahitaji kufikia mafanikio makubwa kwa msimu wa 2020/21.

Chelsea wapo tayari kumuuza nyota wao Jorginho kuliko Kante na hawana habari na wachezaji wawili, ambao wameambiwa watapewa ikiwa ni Eriksen ama Brozovic.







# Chelsea kumtoa kwa mkopo Kepa

**LONDON,** England

CHELSEA ipo tayari kumtoa kipa wao namba moja, Kepa Arrizabalaga kwa mkopo baada ya kumpata mbadala wake, ambaye ni Edouard Mendy kutoka Klabu ya Rennes.

Mendy amepewa mkataba wa miaka mitatu pale Stamford Bridge, baada ya kununuliwa kwa euro milioni 22 na dili hilo lilikamilika Septemba 24.

Kepa amekuwa hana furaha baada ya kufanya makosa wikiendi iliyopita kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, wakati wakipoteza kwa kufungwa mabao mawili, ambayo yalifungwa na Sadio Mane na kuwafanya wayeyushe pointi tatu mazima Uwanja wa Stamford Bridge.

Inaelezwa kuwa, Lampard amepoteza matumaini kwa Kepa licha ya kutoweka wazi kwamba hana imani naye na sababu ya kutaka kumtoa kwa mkopo ni kufanya aweze kuwa imara huko atakokwenda kwa kuwa hatakuwa na nafasi ndani ya kikosi cha Chelsea kwa wakati ujao.

Gary Neville mchezaji wa zamani wa Manchester United na Jamie Carragher mchezaji wa zamani wa Liverpool wamesema kuwa Chelsea haina nafasi ya kutwaa taji la Ligi Kuu England ikiwa itamtumia Kepa langoni kutokana na makosa yake kujirudia.

# Arteta atabiri usajili Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ametabiri Arsenal itakuwa bize wakati wa kufungwa kwa dirisha la usajili, lakini kocha huyo hajazungumza lolote kuhusiana na Houssem Aouar.

Arsenal imekuwa ikihusishwa sana na mbio za kumsajili nyota huyo wa Lyon kabla ya kufungwa kwa pazia hilo Oktoba 5, mwaka huu.

Alipoulizwa kuhusu Aouar baada ya kichapo cha mabao 3-1 kwenye Ligi Kuu ya England kutoka kwa Liverpool, juzi Jumatatu, Arteta hakuwa na jipya lolote kuhusu usajili, lakini alitabiri kuwa kabla ya dirisha kufungwa Arsenal itakuwa bize kwa usajili.

"Hatuna habari yoyote ya usajili wa mchezaji mpya au kuhusu wachezaji kuondoka klabuni kwetu," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Ni wiki, nafikiri tunaweza kuwa bize kwa usajili, ingawa hadi sasa sijui lolote kuhusu mchezaji yeyote mpya, kuja hapa au kuondoka.

"Ngoja tusubiri tuone kitakachotokea."

Arteta aliongeza: "Nafikiri tutakuwa 'bize' kwa usajili. Ingawa lazima niwe mkweli sijui lolote hadi sasa."

Arsenal ilifungwa kwa mara ya kwanza na Liverpool kwenye Ligi Kuu msimu huu na sasa inashika nafasi ya tano katika msimamo.



# SANCHO AKUNWA NA RASHFORD




**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho anayewindwa na Manchester United, amemmwagia sifa mchezaji mwenzake wa timu ya Taifa ya England, anayeichezea miamba hiyo ya Old Trafford, Marcus Rashford kwamba ni mmoja kati ya wachezaji wenye uwezo mkubwa aliowahi kucheza nao.

Inaelezwa, Man United inatarajia kufanya jaribio la mwisho la kumsainisha Sancho kabla ya Oktoba 5, ambapo dirisha la usajili litakuwa linafungwa na dili hilo limekuwa linachelewa kutokana na Dortmund kukataa kupunguza bei ya winga huyo.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, alijiunga na vigogo hao wa Bundesliga Agosti, 2017 akitokea Manchester City.

Katika orodha ya wachezaji, ambao Sancho aliwataja kuwa wana uwezo mkubwa wa kucheza mpira, alimtaja pia David Silva na Kevin de Bruyne miongoni mwa wachezaji watano bora aliowahi kucheza nao.

Alimtaja pia mchezaji mwenzake wa zamani wa Dortmund, Mario Gotze na winga wa sasa wa miamba hiyo, Julian Brandt.

"Nimewahi kucheza na Marcus Rashford na nimeona ana uwezo mkubwa, pia wakati nipo Man City nilicheza na Kevin de Bruyne na David Silva," alisema.

Man United inataka kulipa pauni milioni 90 kwa ajili ya kuinasa saini ya Sancho, lakini klabu yake ya Dortmund inahitaji pauni milioni 108, ili kumuuza mchezaji huyo ambaye amecheza mechi 13 za timu ya Taifa ya England.

# Rudiger agombewa na Barcelona, PSG

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain, West Ham na Barcelona zimeingia kwenye vita ya kuwania saini ya beki wa kati wa Chelsea, Antonio Rudiger katika dirisha hili.

PSG ndiyo inayoonekana kuwa kwenye nafasi kubwa ya kuipata saini yake kwa kuwa ni ngumu Chelsea kuiuzia mchezaji West Ham kutokana na ushindani wa muda mrefu uliopo baina yao.

Katika kufanikisha hilo, PSG imeripotiwa kutaka kumchukua mwamba huyo kwa mkataba wa mkopo, ambao utakuwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja ikiwa ataonyesha kiwango kikubwa.

Mchezaji huyo, ambaye pia anawindwa na Barcelona hayupo kwenye mipango ya Frank Lampard kwa msimu huu.

Mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2022, na thamani yake katika soko la usajili ni Euro 40 milioni. Kukosa kwake namba kunamfanya ajiweke tayari kwenda kuanza maisha mapya kwingineko.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAMFUNGUA MDOMO KLOPP EPL

Haikuwa rahisi, ila nimeona kiwango cha wachezaji ni kizuri wananifurahisha...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool ina jukumu la kuendelea kushinda kila mechi kwenye Ligi Kuu England, ili kutetea taji lao.

**Liverpool, ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Jumatatu usiku waliibuka na ushindi wa mabao 3-1, dhidi ya Arsenal inayonolewa na Mikel Arteta kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Uwanja wa Anfield.**

Arsenal ilianza kuwatungua Liverpool dakika ya 25 kupitia kwa Alexandre Lacazette na bao hilo lilidumu kwa muda wa dakika mbili pekee, kwani Liverpool waliweka mzani sawa kupitia kwa Sadio Mane dakika ya 28.

Wakati Arsenal inayomtegemea Pierre Emerick Aubameyang kwenye upande wa kutupia mabao ikihaha kutafuta ushindi ilitunguliwa bao la pili dakika ya 34 na Andrew Robertson na dakika ya 88 msumari wa tatu ulipachikwa na Diogo Jota.

Hata hivyo, Arsenal watalazimika kumlaumu sana Lacazette, ambaye alikosa nafasi tatu za wazi za kufunga na pengine angeweza kupindua matokeo hayo.

Baada ya mchezo huo, Klopp aliwaambia waandishi wa habari kwamba, ni lazima Liverpool ishinde kila mchezo wa Ligi Kuu ili kutetea taji lao msimu huu.

Klopp alibainisha kwamba ili kufikia malengo waliyojiwekea ikiwa ni pamoja na kushinda tena taji la Ligi Kuu England, kazi yao ni moja kuendelea kushinda mechi zao zote.

"Haikuwa rahisi, ila nimeona kiwango cha wachezaji ni kizuri wananifurahisha wamefanya vizuri na kazi ni moja tu kutafuta ushindi," alisema.

"Jambo muhimu kwetu ni lazima kushinda kila mechi iliyopo mbele yetu, ili kuhakikisha tunatetea taji la Ligi Kuu, vinginevyo kazi itakuwa ngumu sana kwa upande wetu," alisema Klopp.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAKOMAA NA SANCHO

KLABU ya Manchester United haijakata tamaa katika mbio zao za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund raia wa Uingereza, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(ESPN)***

### SPURS YAMWANIA SKRINIAR

TOTTENHAM Hotspur inafikiria kumchukua tena mlinzi wa Inter na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, lakini haiko tayari kumsajili kwa bei inayotajwa. ***(Guardian)***

### BARCA YAMWINDA DEST

KLABU ya Barcelona inakaribia kufikia makubaliano ya mwisho na Ajax kuhusu beki wa kulia wa Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 19, lakini ina uwezo mdogo wa kufanya makubaliano zaidi ya usajili. ***(Goal)***

### UNITED KUMWACHIA JAMES

MANCHESTER United itamruhusu winga wake raia wa Wales, Daniel James, kujiunga na Leeds United kwa mkopo, lakini kama watamsajili Sancho. ***(Sun)***

### LULU EVERTON, LEICESTER

KLABU ya Everton na Leicester City zote zinamnyatia mlinzi wa Chelsea raia wa Ufaransa, Kurt Zouma mwenye umri wa miaka 25. ***(Le10 Sport, via Talksport)***

### BREWSTER AWINDWA SHEFFIELD

SHEFFIELD United imetoa ofa kwa Liverpool ya pauni milioni 17 kwa mshambuliaji wa England, Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 19, na iko tayari kujumuisha kipengele cha kumnunua kwenye makubaliano.***(Sun)***

### BAYERN KUMSAJILI AARONS

KLABU ya Bayern Munich inafikiria kutoa ofa kwa beki wa kulia wa Norwich City, Max Aarons mwenye umri wa miaka 20. ***(Bild)***

### WALCOTT KUTOONDOKA EVERTON

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti hatarajii winga Theo Walcott mwenye umri wa miaka 31, ataondoka katika klabu hiyo kipindi hiki cha usajili. ***(Mail)***

### PEREIRA AWANIWA LAZIO

LAZIO inafanya mazungumzo kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United raia wa Brazil, Andreas Pereira mwenye umri wa miaka 24, kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Telegraph)***

### FOYTH ATAKIWA LAZIO

MLINZI wa Tottenham na Argentina, Juan Foyth mwenye umri wa miaka 22, anawindwa na Valencia. ***(COPE)***

### LEEDS SAFI KWA CUISANCE

LEEDS United iko katika hatua ya mwisho ya majadiliano na Bayern Munich kuhusu kiungo wa kati, Mickael Cuisance mwenye umri wa miaka 21, baada ya raia huyo wa Ufaransa kuiarifu klabu yake ya Ujerumani, kuwa anataka kupata sehemu ya kucheza mara kwa mara. ***(Sport Bible, via Fabrizio Romano)***

### INTER YAJITOSA KWA SMALLING

INTER Milan watajitosa kumsajili mlinzi wa Manchester United na England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, kama watamuuza Skriniar kwa Tottenham Hotspur. ***(Football Italia)***

### SEVILLA KUMUUZA KOUNDE

KLABU ya Sevilla inatarajia ofa ya pili kutoka Manchester City kwa ajili ya mlinzi wake wa pembeni, Jules Kounde na inawezakana wakashindwa kuikataa ofa ya kuanzia euro milioni 65 hadi 70, kwa ajili ya Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

## Karia atangaza neema Mkwakwani

**Na Steven William,** MUHEZA

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limetangaza kuandaa mchakato wa kujenga upya Uwanja wa CCM Mkwakwani uliopo jijini, Tanga ili kufikia vigezo vya kimataifa, imeelezwa.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wadau wa soka wa mkoa wa Tanga akiwamo Mkurugenzi wa Hoteli ya Tanga Beach Resort, Hamisi Kindoroko na Katibu wa CCM (Muheza), Mohamed Moyo.

Karia alisema tayari ameshazungumza na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella na wadau wengine ili kuanza maandalizi ya ukarabati wa uwanja huo ambao utasaidia kuinua kiwango cha wachezaji wa jijini hapa.

Alisema sasa hivi wanatarajia kufanya mazungumzo na uongozi wa CCM Mkoa wa Tanga ili kupata ridhaa ya kuanza mchakato huo kwa sababu wao ndio wamiliki wa uwanja.

" Tunataka kuona uwanja wa Mkwakwani unakarabatiwa na kuwa wa kisasa kabisa ili mechi za kimataifa ziweze kuchezwa katika uwanja huo wa siku nyingi, kama mnavyojua Tanga ni waja leo waondoka leo," alisema Karia.

Katibu wa CCM (Muheza), Mohamed Moyo, alisema wanamshukuru Karia kwa maandalizi yake ya kujenga upya uwanja wa Mkwakwani na kumwomba pia kuutizama na Uwanja wa Jitegemee ambao pia unahitaji matengenezo.

## Coastal yaandaa mipango mipya

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Coastal Union chenye makao yake makuu jijini Tanga, kinatarajia kuwapa wachezaji wake mazoezi magumu kuelekea mchezo dhidi ya Yanga kwa sababu wanafahamu ubora wa wapinzani wao hao, imeelezwa.

Yanga inatarajia kuikaribisha Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema wameamua kubadilisha aina ya mazoezi kutokana na kutambua ugumu wa mchezo huo unaofuata na kuongeza hawataki kurudia makosa waliyofanya kwenye mechi tatu za kwanza.

"Kwa sasa nimeamua kuwapa wachezaji wangu mazoezi maalumu ambayo naamini yatawasaidia tutakapokutana na Yanga, tunaomba mashabiki wetu wazidi kutuunga mkono, kwani kazi ndio imeanza," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema baada ya jana asubuhi kuwapumzisha wachezaji wake, jioni walitarajia kuendelea na mazoezi ya kutengeneza muunganiko ili kuwaweka kwenye nafasi nzuri ya kutengeneza mashambulizi kama walivyofanya katika mchezo wao uliopita dhidi ya JKT Tanzania.

Aliweka wazi bado anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yaliyopo ili kujiweka mahali salama kwenye msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Bara kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# YANGA YAIKARIBISHA KMKM CHAMAZI KUONGEZA MAKALI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIKA mkakati wa kuongeza makali ya kikosi chake, Yanga inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya KMKM kutoka Zanzibar, itakayopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam leo.

**Yanga inajiimarisha na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaendelea, wakati KMKM inajiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar utakaonza ifikapo Novemba 7, mwaka huu.**

Akizungunza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema timu yake imepata mwaliko wa kucheza mchezo huo na kuukubali kwa sababu wana malengo ya kukiimarisha kikosi chao kabla ya msimu mpya haujaanza.

Msimu alisema kikosi chake kitatua jijini na wachezaji 26 na kumtaja mshambuliaji, Mussa Ali Mbarouk, kuwa atakosekana katika mechi ya leo kwa sababu ni majeruhi.

"Timu inatarajia kuondoka hapa Zanzibar leo (jana), na wachezaji wangu wote tuliowasajili, isipokuwa Mbarouk ambaye alipata majeraha ya mguu akiwa mazoezini," Msimu alisema.

Kocha huyo alisema anatarajia kuwatumia wachezaji wake wote ili kuwajenga na kuwapa uzoefu kutoka kwa timu hiyo kongwe na yenye wachezaji wa kimataifa kutoka nchi mbalimbali.

"Wenzetu ni wazoefu na wana wachezaji wazuri, ila lengo letu kwa pamoja ni kuhakikisha timu inacheza vizuri na kukiandaa kikosi chetu kuelekea michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo msimu huu itakuwa na ushindani zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza baada ya kumaliza mechi hiyo, ikirejea Zanzibar itacheza michezo mingine ya kirafiki ili kukubali mialiko kutoka kwa klabu nyingine za visiwani humo.

Yanga itatumia mechi hiyo kama sehemu ya maandalizi ya mechi Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

KIKAZI ZAIDI...



Ofisa Habari wa Klabu ya Simba, Haji Manara (aliyevaa kofia), akiwa katika picha ya pamoja na waandishi wa habari na wafanyakazi wa Kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisaha magazeti ya Nipashe na The Guardian, wakati alipotembelea ofisi hizo Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, kwa ziara ya kikazi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Buriani Mabera, miaka 47 ndani ya Msondo*

**Na Sabato Kasika**

SASA ni wazi kwamba, wakongwe wa muziki wa dansi ndani ya bendi ya Msondo Ngoma wameisha, hii ni kufuatia kifo cha mpiga solo mkongwe nchini, Said Mabera 'Dk. Mabera' (picha) kama ambavyo mashabiki walizoea kumwita.

Kifo chake kimethibitishwa na mwanawe, Mabera Said ambaye alisema baba yake alifariki dunia usiku wa kuamkia jana nyumbani kwao Goba jijini, Dar es Salaam.

Mtoto wake huyo alisema, kifo cha baba yake kimetokana na kuugua kwa zaidi ya miezi miwili, hali iliyosababisha asionekane kwenye maonyesho mbalimbali ya bendi hiyo.

Kifo chake kinaweza kuwa kimehitimisha idadi ya wanamuziki wakongwe wa bendi hiyo waliotangulia mbele ya haki, wakiwamo, Maalim Muhidin Gurumo, TX Moshi William, Suleiman Mbwembwe na Athman Momba (waimbaji).



Wakongwe wengine wa Msondo Ngoma waliotangulia mbele ya haki ni waimbaji, Joseph Maina na Shaaban Debe pamoja na mpiga besi, Suleiman Mwanyiro, hali inayoifanya bendi hiyo sasa kuwa na wanamuziki wengi vijana.

Historia inaonyesha kuwa 'Dk.Mabera' aliyezaliwa mwaka 1949 mkoani Kigoma, na alijiunga na bendi hiyo mwaka 1973 wakati huo ikiitwa JUWATA Jazz wakati akiwa anapiga tarumbeta, ingawa pia alikuwa ni mkung'uta solo. Hakuanza kazi kwa kupiga solo, kwa kuwa alikuta kuna mpiga gita hilo, Abel Baltazar, ambaye baadaye mwaka 1977 alikwenda kuanzisha bendi ya Dar International na hivyo 'Dk. Mabera' akahamia kwenye solo.

Baada ya Baltazar kuhama, wimbo wa kwanza ambao Dk. Mabere alipiga solo ndani ya Msondo ulikuwa ni 'Mpenzi Zarina' na tangu wakati huo, hakuwahi kuihama bendi hiyo hadi umauti ulipomkuta juzi.

Msimamo wake huo wa kutohama katika bendi hiyo, umemwezesha kupata tuzo mbalimbali ikiwamo Hall of Fame, ikiwa ni ya heshima binafsi kwa kudumu bila kuhama aliyotunukiwa mwaka 2011.

Alikabidhiwa tuzo hiyo katika usiku wa Kilimanjaro Music Awards kwa kutambua mchango wake kwenye muziki wa dansi bila kuhama ovyo kama wafanyavyo baadhi ya wanamuziki nchini.

# Michezo

Jumatano Septemba 30, 2020

Nipashe




Arsenal yamfungua mdomo Klopp EPL UKURASA 22

IKO HIVI...



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara (kulia), akizungumza na Kitengo cha Habari za Michezo cha Kampuni ya The Guardian Limited, wachapishaji wa magazeti ya Nipashe na The Guardian, wakati alipotembelea ofisi za kampuni hiyo, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana, kwa ziara ya kikazi. Kulia kwake ni Mhariri wa Michezo Nipashe, Isaac Kijoti na Msaidizi wake, Somoe Ng'itu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Miquissone sasa kuitajirisha Simba

## ●●● Usajili wake watingisha, yakataa shilingi bilioni moja kumuuza, Mo Dewji ataka...

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO wa kimataifa wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaa, Luis Miquissone, ametajwa kuwa ndiye mchezaji ghali kwa sasa sokoni kwa Ukanda wa Afrika Mashariki, imefahamika.

**Ingawa Simba yenye makao makuu yake Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini, haikuwa tayari kutaja kiasi cha fedha ambacho wametumia kumsajili mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Msumbiji, imesema kumuuza kwa Euro 400,000 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni moja bado ni hasara kwao, huku ikieleza inaweza kukubali kukaa mezani kusikiliza ofa kama klabu itakayomhitaji itafika Euro milioni moja (Sh. bilioni 2.6).**

Simba ilimsajili nyota huyo wa zamani wa Orlando Pirates ya Afrika Kusini, Miquissone akitokea UD Songo ya Msumbiji, ambapo alifunga bao lililowaondoa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, akiwa na klabu hiyo.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili zilizoko Mikocheni jijini Dar es Salaam alipotembelea jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema klabu yake ilimsajili Miquissone kwa dau la juu na uamuzi huo ulifikiwa baada ya kuridhishwa na kiwango alichokionyesha kwenye mechi mbalimbali.

Manara alisema waliangalia uwezo wa Miquissone katika mechi mbalimbali alizocheza akiwa na kikosi cha Msumbiji, Orlando Pirates na UD Songo na kuvutiwa na kipaji chake.

"Tunajivunia kuwa na kikosi imara, kwa sasa Miquissone ndiye mchezaji ghali, na si kwa Simba tu, ni kwa Afrika Mashariki nzima, tumemnunua kwa dau nono, halijawahi kutokea, analipa kwa kile kiwango anachokionyesha," alisema Manara.

Aliongeza klabu mojawapo ya Uholanzi ilionyesha nia ya kumnunua kwa dau la Euro 400,000, lakini Simba haikuwa tayari kumwachia kwa kiasi hicho cha fedha kilichotajwa.

"Kuna mawakala wa klabu moja ya Uholanzi walikuja kufanya mazungumzo na sisi (Simba), tena kwa hela nzuri ya Euro 400,000 ili kumnunua, lakini 'Mo', (Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed Dewji) akasema labda walipe Euro milioni moja (Sh. bilioni 2.6), kiasi walichotaka kwetu ingekuwa hasara," Manara alisema.

Aliongeza kiungo huyo ni mali ya Simba na hajasajiliwa kwa mkopo kama baadhi ya klabu nyingine za hapa nchini zinavyoamini.

"Ni mchezaji wetu halali kwa asilimia 100, tena ana mkataba mrefu, hajaja kwa mkopo, thamani yake ni sawa na kikosi kizima cha ...(hakutaka kutaja cha timu gani), tunamshukuru Senzo (Mazingiza- aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba), alisaidia sana kufanikisha ujio wake, hakuna ambaye anaweza kumpata," Manara aliongeza.

Kiungo huyo alitoa pasi za mwisho tatu kwenye mchezo dhidi ya Biashara United ambapo Simba ilishinda mabao 4-0 na pia alitoa pasi kama hiyo kwa mpira wa kona, Meddie Kagere akifunga kwa kichwa. Hadi sasa ndiye mchezaji anayeongoza kwa pasi za mwisho akiwa nazo nne hadi sasa wakati huu Ligi Kuu ikiwa raundi ya nne.

Mchezaji mwingine ghali anayetajwa katika kikosi cha Simba ni kiungo kutoka Zambia, Clatous Chama, ambaye imeelezwa klabu inayomtaka ijiandae kutoa kiasi cha Sh. bilioni mbili.

# Zlatko na mkakati wa ubora Yanga

**Na Saada Akida**

LICHA ya kikosi chake kutoa 'dozi' katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Zlakto Krmpotic, amesema mkakati wake kwa sasa ni kupata michezo ya kirafiki zaidi, ili timu yake icheze kwa kuzoeana na kupata muunganiko bora na hatimaye kutimiza malengo ya kubeba taji la ligi hiyo msimu huu.

Yanga inatarajia kuwakaribisha KMKM ya Zanzibar katika mechi ya kirafiki itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Zlatko alisema licha ya kushinda katika mechi zao tatu za ligi, wachezaji wake wameonyesha kupambana na kutokuwa na muunganiko mzuri kwa sababu ya kukosa matayarisho ya kuanza kwa ligi hiyo.

Zlatko alisema licha ya kuhitaji muda na kutumia mechi za ligi kutafuta matokeo pamoja na kupata muunganiko, pia mechi za kirafiki wanazocheza zinasaidia wachezaji wake kupata uzoefu na muunganiko mzuri.

"Sasa hivi hatuna muda wa kupoteza, tunatumia mechi za ligi kutafuta matokeo chanya, lakini kujenga kombinesheni kwa wachezaji wangu, pia kutumia muda huu kupata mechi za kirafiki ambazo nazo zitanisaidia kupata kile ninachokitarajia ndani ya kikosi changu," alisema Zlatko.

Alisema kulingana na mapungufu ambayo amekuwa akiyaona katika kikosi chake, kubwa ni suala la muunganiko jambo ambalo analifanyia kazi kwa kupata mechi za kirafiki pamoja na kwenye ligi hiyo.

"Suala la ushambuliaji nalo bado hii inatokana na timu hiyo kutopata muda wa kukaa pamoja, haijalishi tunashinda bao 1-0 kila mechi kikubwa ni kupambana kutafuta pointi tatu zitakazotuweka katika nafasi nzuri na kufikia malengo yetu," alisema Zlatko.

Alisema baada ya ushindi dhidi ya Mtibwa wamerejea nyumbani na leo (jana) asubuhi wameingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Coastal Union.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >